ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa na Rais
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
43.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
44.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
45.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
47.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
48.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
49.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake

50.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Jimbo la Kikwajuni

51.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk Jimbo la Kitope

52.Mhe. Marina Joel Thomas Kateuliwa na Rais

53.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

54.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

55.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

56.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

57.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

58.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

59.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

61. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

66.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

69.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

70.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

71.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

76.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Tatu – Tarehe 12 Oktoba, 2012

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe.Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 45

Uchafu katika Maeneo ya Mji Mkongwe

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mji Mkongwe ni hifadhi ya Kimataifa na urithi unaoingizia nchi yetu kipato cha fedha za kigeni, kutokana na biashara ya utalii, lakini mji huo umekithiri uchafu kiasi ambacho hao watalii baadhi ya mitaa wanapopita huziba pua kutokana na harafu mbaya ya uchafu uliozagaa.

Je, Serikali kupitia Baraza la Manispaa wanachukua jitihada gani kuusafisha na kuuweka mji huo katika hali ya usafi muda wote ili utoe taswira inayolingana na hadhi ya Mji Mkongwe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:- Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 45 kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba niwapongeze sana wafanyakazi wetu wa Mji Mkongwe na wengineo wanaofanya au wanaodumisha mambo ya usafi. Na naomba kidogo nisikubaliane na Mhe. Mwakilishi anapozungumza kwamba inabidi wakipita Mji Mkongwe wabane pua kwa kunuka Mji Mkongwe si kweli kabisa, Mji Mkongwe tunajitahidi kwa uwezo wetu na wafanyakazi wetu na watalii kama alivyosema wengi tu kila uchao watalii wengi hawakimbii. Na yeye kama mkaazi wa eneo la Mji Mkongwe ninamuomba tusaidiane kuwashajiisha watu wafuate taratibu za usafi, sote tufanye kazi kwa pamoja. Sasa baada ya maneno hayo ya utangulizi naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, kwa kuongeza uwezo wa kukusanya taka hizo juhudi tunazochukua moja ni kuongeza uwezo kwa kukusanya taka kwa kununua vifaa vya kuhifadhia pamoja na kubebea taka vikiwemo makontena ya taka 193 (*Solid Wastes skips*) na gari saba za kuchukulia makontena kwa Mji wa Unguja, *dust bins* 1,500 na mikokoteni 50 (*Push carts*) kupitia mradi wa kuimarisha huduma za mjini (ZUSP). Yaani mradi huu tumeuomba wenyewe baada ya kuona uwezo wetu mdogo wa kuhudumia mji na tunashukuru Benki ya Dunia wakaitikia ombi letu ndio tukapata msaada huu. Kwa hivyo ni jitihada mojawapo kubwa sana kwamba tumeona uwezo wetu ni mdogo tukaomba msaada na Benki ya Dunia wametuitikia msaada huo.

Lakini pia kuwashirikisha wananchi kwa kutumia vikundi vya jamii na vya mazingira viliopo katika Shehia na Polisi jamii kwa mashirikiano na Manispaa katika kuimarisha huduma za usafi wa Mji, maeneo ya masoko na maduka kwa kufanya usafi wakati wa usiku.

Pia kushirikiana na Waheshimiwa Wawakilishi,Wabunge, Madiwani na Masheha katika kuhamasisha wananchi kuheshimu kanuni za usafi wa Mji za Manispaa na kulipa ada za huduma za taka mjini ili kuinua uwezo wa Baraza la Manispaa katika kutoa huduma endelevu.

Vile vile juhudi ambazo tunazifanya kuhamasisha jamii kushiriki kampeni ya operesheni ya usafi wa Mji wetu kila Jumamosi ya wiki ya mwanzo kwa kila mwezi katika kusafisha maeneo yao. Hizi ni juhudi ambazo tunazichukua kusaidia au kuharakisha au kuzidisha usafi katika Mji Mkongwe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri na ya kutia moyo nimpongeze kwa hilo na nimpongeze zaidi Mkurugeni wake wa Manispaa kwa kazi nzito ambayo ameifanya tusimseme kwa ubaya tu lakini ameshafanya mengi mazuri kwa kweli tunayaona tusimhukumu kwa mengine ni Mkurugenzi wa mwanzo ninapofungua jicho mimi kumuona kwa jitihada anazochukua, naomba unipelekee salamu hizo.

Pamoja na hayo Mhe. Waziri Mji Mkongwe umekuwa ni kivutio kikubwa cha watalii na kitovu lakini sehemu ya marikiti ukipita wakati wa magharibi Mhe. Waziri panachanjwa samaki chini na madamu yanabaki pale na wapita njia inakuwa ni usumbufu kwao.

La pili kuna jitihada gani kutokana na soko lile hivi sasa kuwa kila tukilipigia kelele Wawakilishi imekuwa mtihani, je utakuwa uko tayari kubinafsisha soko lile kumpa mtu kuliendesha ili usafi upatikane.

Tatu, kwa kuwa Mji Mkongwe imekuwa kila jambo wanataka walifanye wao Mamlaka ya Mji Mkongwe na nimekuwa nikilizungumza sana hapa Barazani kuna taasisi mbili kati ya Mamlaka ya Mji Mkongwe na Manispaa zinagongana katika utendaji huo ushahidi upo Mhe. Waziri ukiutaka nitakupa mimi. Je, huoni ule Mji Mkongwe ukawaachia wenyewe wakaendesha usafi ule, maana kodi za milango zinalipwa Mji Mkongwe, kibali Mji Mkongwe, mti ukitaka kukata ndani unaambiwa eneo la Mji Mkongwe, barabara mwisho unaambiwa za Mji Mkongwe.

Mhe. Waziri huoni kuwa hivi sasa umeshafika wakati kuwakabidhi eneo lile Mji Mkongwe tukawapa madaraka hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, suala la Marikiti Mhe. Jaku atakubaliana na mimi serikali kupitia Baraza la Mji tunajitahidi sana kuweka utaratibu uliopo lakini ndio sisi hatutii amri ziliopo. Tukiwakamata wafanyakazi wetu wanapigwa mawe, wanatukanwa, wananyanyaswa. Tukitumia nguvu mnasema aste aste mabaraza ya miji mengine kama Moshi hilo linalosifika kwa usafi wanatumia FFU kabisa kuondoa wamachinga wale. Lakini sisi tunasema jamani tunawapa *lecture* kidogo watii amri ziliopo. Hao unaozungumza wanaopanga samaki barabarani hawaruhusiwi si eneo lake lile eneo la kuuza samaki lipo ndani, lakini sasa mimi ningekuomba sana kama Mwakilishi kwa kushirikiana na Wawakilishi wengine, twenye dhamana ya watu tusaidiane kuelimisha watu. Haipendezi kutumia nguvu ndio sie sie, lakini ikibidi basi tutafanya hivyo. Lakini sheria zetu zipo tunawaelimisha wanazifuata.

Kwa hivyo vurugu unayoiona pale tatizo ni hilo wale wote hawaruhusiki kabisa. Sasa tunajitahidi kuwatumia askari wetu wa Baraza la Mji kuwaelimisha wafuate taratibu ziliopo.

Kuhusu ubinafsishaji kama nilivyosema mara nyingi tu sisi kama serikali hasa katika suala la usafi, tumeshatangaza sera zetu kwamba tunaruhusu hata kuyaendesha masoko, usafi, watu wajitokeze tuko tayari kushirikiana nao kwa njia mbali mbali za ubinafsishaji. Ikiwa hiyo inayoitwa *PPP* au njia nyengineyo, kwa ubia lakini tuko tayari masoko yale kwa kuyaendesha kwa kubinafsisha kwa njia mbali mbali zilizopo, wajitokeze watu tutashirikiana nao.

Halafu suala la mwisho Mamlaka ya Mji Mkongwe, nikiri kwamba ni kweli kuna mivutano kwa kiwango fulani kati ya Baraza la Manispaa na Mamlaka ya Mji Mkongwe. Na labda niseme ni muingiliano kidogo wa baadhi ya kazi. Lakini ninachokuhakikishia kwamba tunajitahidi kukaa pamoja na Mhe. Waziri mwenzangu, wizara ya Maji, Nishati na Ardhi kukaa pamoja Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban tuone tunayatanzua vipi haya matatizo.

Nitatoa mfano tu, uendeshaji wa bustani ya Forodhani, kuna matatizo bustani haiendi vizuri na iko chini ya Bodi maalum ambayo inaundwa na wajumbe kutoka Mji Mkongwe na kutoka Baraza la Manispaa. Kwa hivyo tunajitahidi kukaa pamoja kwa kushirikiana kuwa tunayatanzua hayo matatizo, lakini kama kuna mambo ya kisheria basi serikali itachukua mkondo wake tutayarekebisha hayo mambo ya sheria. Lengo letu ni kuweka sawa mambo, kwa hivyo hiyo migongano midogo midogo tutaiondoa tu kwa kushirikiana.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ninakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kuwa kuuliza swali la nyongeza. Na ninawashukuru wananchi wa Bububu kwa kunichagua.

Kama tunavyojua Mji Mkongwe ni mji ambao unatembelewa na watalii wengi, na serikali inapatikana mapato mengi kutokana na utalii na pale Mji Mkongwe ni kivutio cha watalii. Pale Mji Mkongwe pana majaa mangapi na kuna *zone* Ngapi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kwanza naomba kumshukuru sana Mhe. Husein Ibarahim Makungu Mwakilishi wetu wa Jimbo la Bububu kwa kunipa heshima kubwa kwa kuniuliza swali lake la kwanza mimi.

Mheshimiwa kama nilivyosema juhudi zetu za kusafisha tumeugawa Mji Mkongwe katika *zone* kama nne. *Zone* ya Kaskazini, *zone* ya Kusini, *zone* ya Kaskazini na z*one* ya Mashariki. Hizo zone kila zone ina jumla ya wafanyakazi wake siwakumbuki wangapi lakini hizo ndio juhudi zilizoulizwa katika suala la msingi na tumewagawa hao wafanyakazi wapo wa kudumu katika sehemu hizo. Kwa hivyo wanajitahidi sana kama nilivyosema sikumbuki kila idadi ya *zone* lakini zone ziko nne na majaa *figure* kamili sinayo, lakini ninachotaka kusema kwamba tumegawa sehemu mbili.

Kwanza majaa yale madogo madogo ya kukusanyia na majaa makubwa ambayo yanakwenda kuchukuliwa makontena, lakini hesabu kamili sinayo hiyo nitaitafuta nitakuja kumpatia Mheshimiwa na Waheshimiwa wengine kwa ujumla.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika na mimi kuweza kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri pamoja na majibu yako mazuri ukienda nchi za nje wanakwambia kwanza kodi halafu mazingira. Je wewe Mhe.Waziri huoni iko haja kwa hawa watu wanaofanya biashara pembezoni tukawatoza kodi kwanza halafu tukajali mazingira.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, kwa kweli ninamshukuru sana kwa swali na wazo lake Mhe. Mshimba kwamba tukiweka kodi nzuri ninafikiri hawa wanaohalifu sheria wenyewe watajiondoa. Kwa hivyo ninakubali ushauri wake tutaufanyia kazi.

Nam. 23

Vita dhidi ya Malaria

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Naipongeza Serikali kwa juhudi zake za kutaka kuifanya Zanzibar kuwa ukanda usio na malaria (*malaria free zone)* na kwa kushirikiana na nchi Wahisani kuweza kutupatia vifaa vya kujikinga na malaria kama vile vyandarua pamoja na kutupulizia dawa majumbani. Na kwa kuwa dawa zinazotumika kutibu malaria, dozi yake ni kubwa na inachukua muda mrefu (*long acting*).

Je, ni lini Serikali itatuletea dawa za kutibu malaria zikiwa na dozi ndogo na zinazotibu kwa muda mfupi (*short acting drugs*).

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake nambari 23 kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba nitoe ufafanuzi wa maneno yaliyotumika katika suali hili kwa faida ya Baraza lako tukufu na wananchi wanaotusikiliza.

"Long acting drugs" - dawa inayokaa muda mrefu mwilini bila ya kupoteza nguvu zake kwa mfano, Dawa ya *Amodiaquine* ambayo inatumika kwenye kutibu malaria.

"Short acting drugs" neno hili lina maana ya dawa inayokaa mwilini kwa muda mfupi ambayo haizidi masaa sita na kuhitaji kuongezwa mwilini ili ifanye kazi vizuri, mfano ya nyingi tu za *anti biotic* dawa za kuua vidudu ambazo

huwa hazizidi masaa sita. Na mfano labda mzuri ningeweza kuutumia watu wanapougua *pneumonia* huwa wanapigwa sindano kila baada ya masaa sita. Kwa hivyo hizo tunaziita *short acting drugs.*

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe.Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, dozi ni kipimo cha dawa ambacho kinakadiriwa kutokana na umri na uzito wa mgonjwa ndio kitu dozi. Kwa hiyo dawa za malaria zinazotumika zinazotumia utaratibu huo. Ili nchi iweze kubadilisha dawa inayotumika kutibu maradhi kama vile malaria kuna vigezo maalum vimewekwa na shirika la Afya ulimwenguni,

Vigezo vyenyewe ni kama ifuatavyo:-

a) Madhara makubwa katika jamii
b) Kutokuwa na uwezo wa kutibu *"Resistance"* dawa ambayo imetumika kwa kipindi halafu ikawa haitibu, yaani iwe na *resistance.*
c) Gharama kubwa kuliko uwezo wa nchi.

Hivyo ndivyo vigezo ambavyo vimewekwa na Shirika la Afya Ulimwenguni ambavyo vinatakiwa nchi ivizingatie.

Kwa vigezo hivi dawa za malaria zinazotumika hapa nchini kwetu hazijafikia kigezo hata kimoja kati ya hivyo, kwa hiyo hatuna sababu ya msingi ya kuibadilisha dawa inayotumika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya naomba niulize swali moja la nyongeza lenye vipengele (a) na (b)

a) Kwa kuwa kumekuwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia siku hadi siku, na kwa kuwa siku za nyuma kidogo wataalamu walimudu kututengenezea dawa za *chloroquine* ambayo dozi yake ilikuwa ndogo sana 4 tu hata uwe na umri gani unakula dawa 4 na pale pale ina-*act* kwa maana ni *short acting drug* ukimwagika jasho homa inafifia. Je, ni sababu gani ambazo wataalamu sasa hivi wametuletea hizi dawa za mchanganyiko ni dawa nyingi unatumia yaani huku ukichukulia kwamba *any drug is poison.* Ni sababu gani wameziondosha *chloroquin* ambazo tulikuwa tukila kidogo tu unapata nafuu, leo wametuletea hivi dawa za mchanganyiko ambazo tunakula nyingi sana, jambo ambalo linaleta athari zaidi kwa afya zetu.

b) Kwa sababu kukinga ni bora kuliko kutibu siku zote Mhe. Naibu Spika, na kwa kuwa serikali yetu ya GNU kupitia nchi wafadhili inajitahidi kutupa vyandarua ili kuweza kujikinga na malaria, vyandarua ambavyo baadhi ya wananchi mpaka sasa hivi wanaviweka masandukuni hawavitumii, jambo ni tatizo sana. Je ni hatua gani iliyochukuliwa na serikali ili kuhamasisha wananchi wale vyandarua vile kuvitumia badala ya kuweka masanduku yao au chini ya michago.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, maneno aliyoyazungumza yana ukweli, zamani tulikuwa tunatumia *quinine* ambavyo ni vidonge vinne na vinatumika mara moja baada ya hapo mtu anapona. Lakini ninachotaka kwanza afahamu kwamba kutumika vidonge vinne kwa mara moja haimaanishi kwamba hiyo ni *short acting* unayoizungumza. Kama nilivyosema kwenye suala langu *short acting* ni ile dawa inayokaa mwilini kwa kipindi kifupi. Quinine vidonge vinne si *short acting* isipokuwa inatumika mara moja. Labda unachokisema hapa ni ule usumbufu wa kutumia dawa kwa siku tatu na usumbufu wa kutumia dawa kwa siku moja.

Sasa kutumika dawa kwa siku tatu haina maana kwamba *long acting* na kwa siku moja ni *short acting.* Kwanza tufahamiane hapo. Sasa katika matibabu WHO nayo ina miongozo yake, tunapokuwa tunatibu maradhi huwa kuna dawa *first line* na *second line.* Dawa za *first line* zinatakiwa zitumike na yule ikishindikana kutibika kwa dawa hizo ndipo *second line* inapotumika.

First line ya dawa za malaria ni dawa za *artesunate* na mchanganyiko mwengine wa dawa nyengine. Kwa mfano hapa kwetu tunatumia *Amodiaquine* pamoja na *artesunate* hizo ni kama *first line.* Ikishindikana hiyo kumtibu mgonjwa ndipo inapotumika s*econd line. Second line* ni *quinine* hivyo ndivyo ilivyopangwa. Huwezi kuja mtu kwa

mara ya kwanza tu ukampa vidonge vya *quinine* ukaanza kumtibu ili apate kula dawa kwa siku moja bila kuanza na *first line*.

Na hata hiyo *quinine* ikiwa ni *second line* nayo humtibu kwa siku moja anatibiwa kila baada ya masaa 8 mgonjwa ule anakula kwa muda wa siku 7 na hiyo ni *second line*. Kwa hivyo hiyo quinine walivyokuwa wakipewa zamani baada hiyo teknolojia unayoisema hivyo ndivyo ilivyofikia kwamba iwe ni *second line* na inatumika siku 7 kwa masaa 8. Ina maana masaa manane kwa siku ina maana kwa siku mara 3 kwa masaa 24 kwa muda wa siku 7 ndipo itapoweza kufanya kazi.

La Pili umezungumzia *chloroquine*, ninafikiri katika vigezo ulivyovizungumza tumesema dawa ambayo ime-*develop resistance* haiwezi ikatumika. Kwa tafiti zilizofanyika Zanzibar ilifikia kiwango cha kuwa *chloroquine* haitibu tena malaria, kwa hivyo ndio maana ikaondoshwa zikaletwa dawa nyengine. Kwa hivyo *chloroquine* haitoweza kutumika tena hapa kutokana na tafiti zilizofanywa kuonesha kwamba wananchi hawaponi kwa dawa zile.

Dawa mchanganyiko, kwa nini dawa mchanganyiko tunatumia *artusenate* tunatumia *amodiaquine*. Katika hizi biotic na dawa zote zinazotumika sasa ulimwenguni imekuwa imehakikishwa kwamba dawa zikitumika mbili kwa wakati mmoja hizo zinakuwa na nguvu zaidi kwa sababu huwa zinafanya kazi mbili tofauti.

Kwa mfano dawa ya malaria ambayo ina *artisunate* na *amodiaquine*, *artisunate* inafanya kazi ya kusafisha wadudu wa malaria kwenye damu kwa haraka sana. Kwa hivyo mtu akipata *artisunate* siku moja tu siku ya pili homa inashuka. Lakini *amodiaquine* inafanya kazi kwenye ini kwa sababu huko ndiko wadudu wa malaria wanakokua wanatunzwa na kuanza kuzaliwa. Kwa hivyo kinachotendeka pale kwa *amodiaquine* ni kuhakikisha kwamba inasafisha dawa kwenye ini. Kwa hivyo mgonjwa anapotibiwa na dawa hizo mbili tu zinasafisha wadudu kwenye damu na kwenye ini na ndio maana baada ya hapo inamchukua muda mgonjwa yule kuugua malaria. Lakini ukiwa utamtibu kwa dawa moja tu labda *artisunate* ambayo iko kwenye damu na ini hatukulishughulikia baada ya muda mfupi wadudu watazaliwa na mgonjwa anapata homa tena.

Kwa hivyo kutumia kwa dawa mbili kunamaanisha kwamba tunajitahidi kuhakikisha kwamba mgonjwa yule asirudiwe na maradhi yale, labda baada ya muda atakapoumwa tena na mbu na haitachukua muda kwa sababu mbu akishamuuma mgonjwa hawa wadudu wanakwenda kwenye ini, akaenda kwenye ini anakutana na dawa. Kwa hivyo hilo ndio tatizo linapotokea. Kwa hivyo hivyo ndio dawa zinapofanyishwa kazi. Na ndio maana tumechagua *amodiaquine* na *artisunate* katika matibabu ya dawa zetu.

Suali la pili linahusu vyandarua. Mhe. Naibu Spika, vyandarua vimegawanywa, serikali imegharamika, watu wanavitia masandukuni ndivyo anavyosema Mwakilishi, kwa nini watu hatuwahamasishi na watu wanavitia vyandarua masandukuni. Watu wamehamasishwa vya kutosha kuhusu masuala ya kutumia vyandarua. Kuna watu tu wenyewe kwa hisia zao hawapendi kutumia vyandarua, anaweza kupewa chandarua lakini asijifunike. Wengine wanasema wakijifunika chandarua unajihisi kama uko kwenye kaburi, kwa hivyo unajiona kama umezongwa, wengine tu hawapendi wanapenda kulala wakiwa wazi, wengine wana visingizio vya joto mradi visingizio viko vingi.

Lakini suala la kusema kwamba watu wanavitia vyandarua kwenye masanduku hilo linahitaji utafiti, mimi utafiti huo sijausikia, kama umefanyika na watu wametia vyandarua kwenye masanduku. Kwa hivyo sina uhakika kwamba vyandarua vimetiwa kwenye masanduku. Labda kama wewe una ushahidi wa kutosha tupe kama utafiti umefanywa ukaonesha kwamba vyandarua watu wangapi wamevitia kwenye masanduku na watu wangapi wanavitumia. Sisi utafiti huo hatujafanya kwa hivyo ninaamini kwa elimu iliyotolewa watu vyandarua wanajifunika, kwa sababu wameelezwa sababu kwa nini wajifunike malaria. Sasa hivyo vya kutia sandukuni mimi sijui.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri suali moja la nyongeza. Mheshimiwa kutokana na kuvutika sana na majibu yake, na kwa kuwa wananchi wengi sasa hivi wameanza kuonesha kuzisusia hizi dawa mchanganyiko kutokana na athari yake mtu akishakula anahisi kama moyo unataka kusimama au vyenginevyo, lakini kumbe baada ya maelezo yake zinaonekana hizi dawa zina umuhimu mkubwa sana.

Sasa haoni Mhe. Naibu Waziri kwamba kuna haja ya kutufanyia semina sisi Waheshimiwa Wawakilishi ili tukajua kwa udhati kabisa faida ya dawa zile na hatimaye sisi tukenda majimboni kuwahamasisha watu kutumia dawa hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza ningependa kutoa maelezo kidogo kuhusu hilo analolisema. Tunapozungumza kwamba hizo dawa zina matatizo au zinawapa taathira watu ni kweli kwa sababu labda inaweza kuwa moja katika mawili, aidha mtu anaelekezwa hafuati maagizo au wanaozitoa dawa hawatoi maelekezo. Kwa sababu, dawa ya *Amodiaquine* ikitumika mwilini kinachotendeka ndani ya mwili baada tu ya kutoa wadudu kule kwenye ini kazi nyengine ili kufanya hiyo kazi sukari inatumika sana ndani ya mwili. Kwa hivyo mtu anapokula *Amodiaquine* sukari inashuka na hicho ndicho kinachomfanya mtu ajisikie vibaya hiyo ndio *side effects* moja ya *Amodiaquine*

Kwa hivyo, mtu anapokula dawa za malaria anashauriwa anywe maji kwa wingi na anywe vitu vya sukari kwa wingi ili kuhakikisha kwamba ile sukari inayotumika ipande kwenye mbili na asipofanya hivyo ndio anapojisikia vibaya, sukari imeshuka na kujisikia kizunguzungu. Anapopelekwa hospitali kinachofanyika ni nini? Wanamtundikia tu sukari *glucose* anainuka anakwendazake. Kwa hivyo, naomba wananchi wafahamu kwamba unapotumia dawa za malaria jitahidi mnywe maji kwa wingi na vitu vya sukari ili kuondosha hilo tatizo, sio tatizo ambalo haliwezi kuepukika, linaweza kuepukika ikiwa tutafuata huo utaratibu. La pili nitawashauri watu wa malaria waandae semina tuje tulizungumze hilo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi asubuhi hii kuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b).

(a) Pamoja na majibu yake mazuri sana Mhe. Naibu Waziri, lakini Zanzíbar imetangaza kuwa malaria hakuna. Je, hii lugha ni sahihi.

(b) Kulikuwa na mradi maalum kuwa mtu anapokwenda kupima malaria huwa analipwa. Je, mradi huu umepotelea wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, tumetangaza Zanzíbar kuwa ni *free of Malaria*. Katika kutangaza tangazo kama hilo kunamaanisha mambo mawili, unaweza ukasema hivyo wakati vatu wanapofikia kitu kinachoitwa *eradication, eradication* inamaanisha kwamba ule ugonjwa umeshuka kwa kiwango cha chini sana. Kiwango cha malaria tulichonacho sasa hivi Zanzíbar ni 0.6 ni chini ya 1 hao ndio wanaougua malaria. Kwa hivyo, kwenye *level* ya *eradication* tumefikia inamaana kwamba ugonjwa wa malaria Zanzíbar si tatizo tena.

Lakini hatujafikia *elimination* tunapofikia *elimination* inamaana kwamba kuwe hakuna mgonjwa hata mmoja. Mfano labda wa maradhi kama hayo ndui, ndui imeshafikia *elimination* ulimwenguni kwamba hakuna mgonjwa hata mmoja. Lakini Zanzíbar 0.6 ya malaria ipo. Hilo la kwanza.

La pili Zanzíbar kunaingia watu na kutoka, wenzetu tu hapo Bara bado hawajafikia kama tulipofika sisi kwa hivyo wanaweza vatu kutoka kule wakaja huku au sisi wenyewe tunatoka huku tunakwenda kule tunachukua kule tunarudi nayo hapa malaria. Kwa hivyo, bado sisi hatujafikia hilo lengo la ku-*eliminate* na hatutafikia midhali nchi zinazotuzunguka bado zina kiwango cha malaria. Hivyo, nataka kusema kwamba Zanzíbar malaria hakuna kwa utaratibu huo kwamba yameshuka kiasi cha kwamba sasa si tatizo tena kwetu, tunachokifanya sasa hivi tunajaribu tuzuie hapo tulipo aidha tushuke au tusipande hapo. Kwa hivyo hiyo ndio kazi tunayoifanya.

Suala la mradi wa kulipwa mimi tangu nimefika Wizara ya Afya hilo sikulikuta kwa hivyo sina uhakika nalo.

Nam. 50

Kiwango cha Ubora wa Bidhaa Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa muda mrefu limepitia Sheria ya Kuanzisha Shirika la Kusimamia Viwango vya Ubora wa Bidhaa ili kuondoa malalamiko ya kuingizwa bidhaa za chini ya viwango.

(a) Je, sheria hiyo imetekelezwa kwa kiwango gani na serikali hadi sasa.

(b) Kwa kuwa bidhaa nyingi zikiwemo vifaa vya umeme vinaingizwa Zanzibar bila ya kuzingatia ubora. Je, serikali haioni kuchelewa kuanzishwa kwa shirika hilo ni kurudisha nyuma maendeleo ya wananchi wake.

(c) Kwa kuwa shirika hilo linahitaji watu wenye taaluma maalum na wenye uwezo. Je, serikali ina wataalam wangapi wa kuchunguza viwango vya ubora wa bidhaa mbali mbali Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 50 lenye vifungu a, b na c linalihusiana na kuanzishwa kwa Shirika la Kusimamia Viwango na Ubora wa Bidhaa kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nataka nikubaliane naye Mhe. Mwakilishi kwamba, Baraza lako tukufu lilipitisha sheria na ni Sheria nambari 1 ya mwaka 2011 inayohusiana na kuanzisha Shirika la Viwango la Zanzibar, ili kuweka na kusimamia viwango na ubora wa bidhaa zinazozalishwa na kuingizwa Zanzibar.

(a) Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza sheria hiyo, tayari Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amekwishamteua Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo tarehe 30 Agosti 2012. Pamoja na hatua hizo maandalizi ya kiutendaji yameanza kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na Mkurugenzi Mkuu huyo kwenda Tanzania Bara kujifunza namna ya utekelezaji wa majukumu yake katika shirika hilo.

Kwa upande mwengine Mhe. Naibu Spika, tayari serikali imeshatenga bajeti na eneo maalum kwa ajili ya kuanzia shughuli za shirika hilo huko Maruhubi katika eneo lililokuwa kiwanda cha Sigara. Pamoja na hayo, hatua za utayarishaji wa nyaraka za zabnuni kwa ajili ya michoro na ujenzi zinaendelea kuchukuliwa. Aidha, kwa muda huu Mkurugenzi Mkuu huyo anafanyia shughuli zake ndani ya jengo la Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Hatua nyengine zinazoendelea kuchukuliwa ni pamoja na kutayarisha Kanuni, Muundo wa shirika na mpango mzima wa utekelezaji wa shughuli za shirika hilo.

(b) Mhe. Naibu Spika, lilipokuwa nikijibu swali hili katika kifungu (a) kuwa tayari hatua za awali za maandalizi ya uundwaji zimeanza kuchukuliwa tabaan Mhe. Naibu Spika, inapotokezea kupatikana kwa bidhaa zikiwemo za umeme zenye kutiliwa mashaka juu ya ubora wake basi sampuli ya bidhaa hizo huwa zinapelekwa katika Shirika la Viwango la Tanzinia Bara (*TBS*) kwa ajili ya kuthibitishwa ubora wa viwango vyake kabla ya kutumika kama ambavyo Sheria ya Shirika la Viwango la Zanzibar inavyoruhusu kutumia taasisi nyengine ili kuweza kutekeleza majukumu yake.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Shirika la Viwango la Zanzibar ndiyo kwanza limeanzishwa bado halijakuwa na wataalam wake, ingawa kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mashirikiano na Wizara inayoshughulika na Utumishi wa Umma zimo katika kuandaa maandalizi ya utaratibu wa jinsi ya kuwapata wataalamu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Serikali imechukua hatua gani kuwafahamisha wananchi kupitia vyombo vya habari ili kujua umuhimu wa chombo hiki baada ya Mkurugenzi kuteuliwa siku hizi za karibuni ili wafahamu umuhimu.

Pili, kwa kuwa kilio cha wananchi wengi ni vifaa vya umeme. Je, wizara yako itafanya jitihada gani kupitia maduka na maghala kuangalia vifaa hivyo vilivyokuwa hafifu.

Tatu, nikupongeze sana kwa kumpeleka mtaalamu Tanzania Bara kwenda kuangalia, lakini nisikitishwe vile vile tena wizara iko *serious* kweli hakuna pahala pengine pa kumpeleka zaidi ya Tanznia Bara.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, nimesema kwamba tumo katika kuandaa maandalizi ya utekelezaji wa sheria ambayo Baraza lako limepitisha mwaka jana. Mhe. Naibu Spika, katika

maandalizi hayo ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kwamba kuna chombo hiki ambacho tumekianzisha kwa sheria na kwa hivyo kuna haja ya kukitumia katika kuhakikisha bidhaa zinazoingizwa au kuzalishwa nchini zinakuwa na ubora unaostahiki.

Kwa hivyo, nataka kumwambia Mhe. Mwakilishi kwamba miongoni mwa shughuli ambazo zinafanywa sasa hivi katika maandalizi hayo ni pamoja na ku-*create awareness* kwa wananchi (kuwapa elimu).

Mhe. Naibu Spika, vifaa vya umeme pamoja na vifaa vyengine vya ujenzi vinavyoingizwa ndani ya nchi. Vifaa hivi vyote Mhe. Naibu Spika, vinakaguliwa bandarini na nataka nimtoe wasiwasi Mheshimiwa kwamba katika ukaguzi huo endapo inatokea kuna wasiwasi wa ubora wa vifaa hivyo basi huwa tunapeleka Tanzania Bara na ndivyo tulivyokuwa tukifanya kabla ya kupitisha sheria hapa Barazani mwaka jana. Lakini nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba, utaratibu huu tuliokuwa tukiutumia kwa muda wote kwamba pindipo vinatokea vifaa au zana au hata vyakula kuonekana kwamba ubora wake haukidhi haja ile inayostahiki basi huwa tunatumia maabara za wenzetu za *TBS* kule Tanzania Bara. Ingawa tumeanzisha ya kwetu kupitia sheria tuliyoipitisha lakini bado hatujaweza kutoa huduma hiyo kama *ZBS*. Kwa maana hiyo bado tutaendelea kushirikiana na wenzetu wa Tanzania Bara mpaka hapo shirika letu litakapoweza kujitegemea.

Mhe. Omar Ali Shehe: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ili nimuulize Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza lenye sehemu a na b. Katika jibu lake la msingi Mhe. Naibu Waziri alituambia kwamba Mkurugenzi kaenda Tanzania Bara kwa ajili ya kujifunza. Nakumbuka Mhe. Naibu Spika, sheria tuliyoipitisha ilitaja sifa za mtu ambaye angepaswa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi ambapo sheria ilimtaka awe ni mtu mwenye sifa za kukiongoza chombo hiki.

(a) Sasa naomba nijue ni sababu ipi iliyopelekea Mhe. Rais kuteuwa mtu ambaye hana sifa kwa lugha nyengine mwanafunzi katika masuala haya.

(b) Mhe. Naibu Waziri kwenda kwenu mbio katika suala hili kwa kujipanga huoni kwamba kunazidi kuwapa fursa wafanyabiashara waingize vifaa vibovu na hivyo badala ya kuwasaidia wananchi tunazidi kuwafanya kuwa masikini kwa kununua vifaa vibovu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, Mkurugenzi Mkuu aliyeteuliwa na Mhe. Rais ana sifa zote zinazostahiki. Lakini ni kawaida kwamba kwa kazi maalum basi hapana budi na sote humu Mhe. Naibu Spika, pamoja na kwamba ni Wawakilishi bado tumekua tukijifunza jinsi ya kuwakilisha wananchi. Kwa maana hiyo elimu haina mwisho lakini kwa kazi maalum hii ya ubora wa bidhaa basi ni vyema kwenda kujifunza Mkurugenzi huyu akaone kazi hizi zinasimamiwa namna gani.

Nataka nimwambie Mhe. Omar Ali Shehe kwamba, mimi binafsi nimetembelea shirika hili la *TBS* la Tanzania Bara ni shirika kubwa sana na kila siku linaendelea kupanuka katika utendaji wake sisi ndio kwanza tuna anza. Kwa maana hiyo si vibaya kwenda kujifunza kwa wenzetu tuanze vipi ili hatimaye na sisi tuweze kusimama kwa miguu yetu wenyewe.

Lakini Mhe. Omar Ali anataka kujua kwa nini hatuelimishi wananchi kutonunua bidhaa ambazo hazina ubora. Mhe. Naibu Spika, ununuzi wa bidhaa inategemea soko na uwezo wa mnunuzi. Sisi uwezo wetu mpaka sasa hivi ni ku-*control* ndani ya nchi yetu ya visiwa vyetu vya Zanzibar, lakini kutokana na uhuru wa biashara wafanyabiashara wanakwenda kununua nje ya Zanzibar. Kwa hivyo sisi huwa tuna-*control* katika kuingiza ndani ya Zanzibar. Lakini nimtoe wasiwasi Mhe. Mwakilishi kwamba mpaka sasa hivi nashukuru kuwa wananchi wetu wafanyabiashara wanaelewa ubora wa kununua vifaa vyenye vigezo vinavyotakiwa. Ni mara chache sana lakini kwa muda mrefu sana sasa hatujakamata vifaa ambavyo havina ubora hasa vya ujenzi Mhe. Naibu Spika.

Tatizo kubwa linatukuta kwenye vifaa vya chakula lakini vya bidhaa za ujenzi, umeme na vyenginevyo bado ni muda mrefu havijakamatwa lakini tunapokuwa na wasi wasi huwa vinapelekwa Tanzania Bara kuangaliwa ubora wake na kama vinaonekana kwamba vina ubora unaostahiki basi vinaruhusiwa kutumika. Kwa hivyo, namtoa wasiwasi Mhe. Mwakilishi, wananchi wame elimika na wanafahamu na hasa wafanyabiashara.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la mwisho la nyongeza juu ya suala hili. Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake alikuwa anasisitiza kuwa pale ambapo bidhaa

inaonekana kuwa haina ubora tunaipeleka Tanzania Bara kwa uchunguzi. Lakini Mhe. Naibu Spika, mara nyingi tunapokwenda madukani kutaka bidhaa pengine pasi, redio na vyenginevyo mfanyabiashara mwenyewe anakwambia mzee bora hii ni *origin* kuliko hii. Pale mfanyabiashara mwenyewe anakuonesha kuwa hii sio bora na tayari ipo. Je, ni kweli vifaa hivi vinapelekwa huko Bara kwa uchunguzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, nimesema katika majibu yangu Mhe. Naibu Spika, kwamba unununzi wa bidhaa unaendana na uwezo wa mfanyabiashara au mnunuzi au mtumiaji wa bidhaa ile. Mimi nataka nikiri mbele ya Baraza lako Mhe. Naibu Spika, kwamba bidhaa hizi pasi au redio kweli siku za nyuma zilikuwa nyingi hazikidhi viwango na wizara imelifanyia kazi kwa nguvu zote tatizo hili na hivi sasa vifaa hivi havipo katika soko na ni kwa mashirikiano ya hali ya juu na hili Shirika la *TBS* la Tanzania Bara ndio maana tumeweza kupata mafanikio hayo ya kuondoa vifaa hivi visivyokuwa na ubora unaostahiki katika soko.

Kwa hivyo, nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba vifaa hivi sasa hivi ndani ya soko havipo na tofauti ya bei ya bidhaa zozote Mhe. Naibu Spika, inategemeana na kampuni inayotengeneza bidhaa hizo, hata kalamu unaweza kukuta kalamu hii ukaambiwa shilingi mia mbili, nyengine ukiitaka ukambiwa shilingi mia tana na kuna kalamu mpaka shilingi elfu moja na elifu kumi. Vile vile kuna kalamu mpaka shilingi laki mbili inategemea na *material* zinazotumika katika utengenezaji wa bidhaa ile. Kwa hivyo, tofauti ya bei Mhe. Naibu Spika, haipelekei kwamba kifaa kile ubora wake haustahili lakini ni kutokana na *material* yanayotumika katika kutengeneza bidhaa ile.

Nam. 3

Serikali Kushindwa Kuzihifadhi Nyumba za Maendeleo

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Nyumba za Maendeleo ziliasisiwa na kuanzishwa na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume kwa lengo la mkwezi na mkulima kupata hifadhi nzuri ya maisha yake. Na kwa kuwa viongozi wetu wa awamu ya kwanza na ya pili walifanikisha azma hiyo kwa kujenga nyumba za ghorofa na za chini katika maeneo mengi hapa Zanzibar.

Je, ni sababu zipi za msingi zilizopelekea serikali yetu kushindwa kuzitunza pamoja na kuziendeleza nyumba hizi sambamba na kujenga mpya.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 3 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa nyumba za Maendeleo zilijengwa mijini na vijijini Unguja na Pemba na Mzee Abeid Amani Karume kwa lengo la kuwasaidia wananchi wa visiwa hivi kupata makaazi bora. Mhe. Naibu Spika, nyumba nyingi za maendeleo ni kweli kuwa zipo katika hali mbaya na zinahitaji matengenezo makubwa na hii inatokana na kukosekana kwa fedha za kuzitengenezea nyumba hizo, kwani fedha zinazopatikana kwa sasa hivi huwa zinaelekezwa katika ukarabati wa kutengeneza makaro.

Mhe. Naibu Spika, katika jitihada za kuwapatia wananchi nyumba bora na za kisasa, serikali kwa makusudi hivi sasa inaendelea kutayarisha sheria ya uanzishaji wa Shirika la Nyumba, ikiwa ni imani kuwa shirika hilo kuzitunza na kuzienzi nyumba zilizopo. Mbali na Shirika la Nyumba bado serikali inaendelea kuwasiliana na wawekezaji mbali mbali ili kuweza kuwekeza katika ujenzi wa nyumba hizo za makaazi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. naibu Spika, pamoja na majibu mazuri kwa lugha ya kutetemeka ambayo amenijibu Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza lenye kipengele a, b na c.

(a) Kwa kuwa nyumba hizi nyingi zikiwemo zile za ghorofa za Machomane, Madungu, Mwambe, yamo katika hali ngumu hata kushindwa kudhibiti mfumo wake wa maji taka. Je, serikali ina mpango gani wa kuzifanyia matengenezo makubwa nyumba hizi ili kuzinusuru zisianguke.

(b) Kwa kuwa nyumba hizi zilijengwa kwa bidii kubwa ya Muasisi wa nchi hii marehemu Mzee Abeid Amani Karume kwa lengo la kuwapatia makazi bora wakwezi na wakulima. Je, kuziachia katika hali mbaya kama ilivyo sasa si kurudisha nyuma na kuvunja dhamira halisi ya muasisi wa nchi hii.

(c) Kwa kuwa serikali inaonekana haina uwezo kabisa wa kushughulikia nyumba hizi. Je, ina mpango gani wa aidha kuziuza au kuwawekea wawekezaji.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, katika jibu la msingi Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba fedha zinazopatikana sasa ndio mpango uliopo wa kufanyia matengenezo ya makaro na sehemu nyengine za maji machafu katika nyumba hizi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, swali la pili hakuna nia katika serikali hii ya kurejesha nyuma jitihada alizofanya Marehemu Mzee Abeid Amani Karume kwa kuwafikiria wananchi kuwajengea nyumba hizo. Kwa maana hiyo ndio wizara yangu na serikali kwa jumla imechukua hatua mbili, hatua ya kwanza kufikiria kuanzisha Shirika la Nyumba na hatua ya pili ni ile sheria ambayo ilipitishwa na Baraza hili ya *Condominium* ambayo hiyo itawawezesha wanaoishi ndani ya nyumba kuwa na kamati yao ya *Condominium* ambapo wenyewe watakuwa wanaihudumia na wanaiendesha na itakuwa inasaidia kuzifanyia matengenezo nyumba hizi ili hili suala liendelee kuwepo.

Swali la tatu, Mhe. Naibu Spika, suala la kuziuza nyumba hizi ndio linakwenda pamoja na sheria ya *Condominium*. Kwa sababu *Condominium* itawezesha watu wenyewe kutengeneza nyumba zao lakini pia kutengeneza koridoo, ngazi, dari na paa kwa kutumia ile kamati yao ya *Condominium.* Ahsante sana.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa azma ya muasisi wa nchi hii Mhe. Abeid Amani Karume ilikuwa ni kujenga nyumba hizi na kuwapatia makazi bora wakwezi na wakulima. Na kwa makusudi serikali ya Awamu ya Sita iliamua kuzifanyia marekebisho au kuzijenga nyumba hizi zikiwemo nyumba za Mpapa. Je, serikali imejipanga vipi kuendeleza azma ya Marehemu Mzee Karume katika hizi *flat* 24 za Mpapa kwa lengo la kuwapatia makazi wale walengwa na si vyenginevyo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, jitihada za serikali za kuendeleza nyumba hizi sio za Mpapa tu peke yake, lakini hata hili la Michenzani ambalo watu wameshalipwa hivi sasa fidia zao zinaendelea. Mhe. Naibu Spika, sasa hivi serikali ina azma ya kuongeza ujenzi wa nyumba nyengine kwa utaratibu mwengine mpya ambao tutaueleza baadae hatutaueleza hapa leo kwa sababu uko jikoni ndio kwanza unapikwa, lakini nyumba za Mpapa zikimalizika zitakwenda katika utaratibu wa kuwapa wananchi kwa njia ile ile ya kisasa sio ile ya zamani ya nyumba bure, watapangishwa watakaopangishwa, watauziwa watakaouziwa. Ahsante sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kunipa fursa na mimi nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza lako tukufu la Wawakilishi lina kamati zinazofanya kazi kwa wizara zote, na kwa kuwa kamati yako ya Mawasiliano na Ujenzi imetoa ripoti kuhusu nyumba zilizoko Kengeja kuwa ni mbaya, mbaya kupita kiasi, na kwa kuwa nyumba zile zinakaa wananchi na ni juzi tu tulipata msiba mkubwa wa kuzama meli na watu wetu wakafariki, na kwa kuwa nyumba zile zina hatarisha maisha, jee Wizara yako ya Majenzi itachukua hatua gani za makusudi au jitihadi za makusudi kuwahami watu walioko katika nyumba zile za Kengeja ambapo ni mbovu kupita kiasi.

Jee, serikali itachukua juhudi gani ya kuzihami zile nyumba au kuwatafutia sehemu wale waliomo ili wakae na wakati zile nyumba zikifanyiwa maarifa mengine.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji, na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Subeit swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, tunajua tatizo la nyumba za Kengeja lakini nyumba zile za Kengeja karibu zote zinamilikiwa na wananchi isipokuwa nyumba tano ndio za wizara yangu. Lakini hata hivyo wizara ilichukua hatua ya kuziezeka nyumba zile mabati yameibiwa na sasa hayapo kule juu ya paa. Tusaidiane wakati tunapochukua hatua kuzitengeneza hizi nyumba tusaidiane sisi tunaoishi pale na jirani tunaoona tusizifanyie uharibifu.

Mhe. Naibu Spika, uharibifu wa nyumba za maendeleo unasikitisha sana na sina nafasi ya kuzungumza hapa leo, serikali inajenga lakini wakati wanakwenda wanabomoa. Nitatoa mfano mdogo tu. Jumba Na. 10 la Michenzani baada ya kuwagaiya watu kila aliyelipwa fidia nyumba yake zikabakia kama nyumba mbili tatu, hatukumaliza hata mwezi mmoja au miezi miwili tayari nyumba zimeshaibiwa milango watu wameshakwenda kuuza, vitasa vile watu wameshakwenda kuuza, vioo watu wanang'oa, hii ndio hali halisi.

Sisi tunajitahidi kuzitengeneza lakini tushirikiane na Waheshimiwa Wawakilishi kwamba tunapochukua juhudi kwa ajili ya kuendeleza wananchi basi tuendelee na jitihada ya kusaidia kuondoa uharibifu katika maeneo haya.

Nam. 39

Ubomoaji wa Mabanda ya Bandarini

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza**:-**

Mhe. Naibu Sika, katika eneo la mabanda ya Bandari ya sehemu ya abiria kumekuwepo na harakati za kuongeza banda jengine badala ya lile la asili na kubadilisha mazingira ya ramani ya Mji Mkongwe kinyume na masharti ya Uhifadhi ya Kimataifa ya Mji Mkongwe duniani.

(a) Je, Wizara inazungumzia vipi ubomoaji huo na nani amepewa eneo hilo kwa ajili ya kuliendeleza na kubadilisha sura yake ya asili.

(b) Kwa kuwa Serikali kupitia Baraza hili imekuwa ikisisitiza umuhimu wa kuheshimu masharti hayo ya Kimataifa imekuwaje majengo hayo ya asili kubomolewa huku magari yakiwekewa masharti ya kuingia Mji Mkongwe wa Zanzibar.

(c) Kama eneo hilo kapewa mfanyabiashara utaratibu gani umetumika katika masuala ya zabuni kukaribisha ushindani kwa wafanyabiashara wengine kama utaratibu wa Sheria na Utawala Bora unavyoelekeza.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 39 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika,

a) Ni kweli kuwa katika eneo la mabanda ya Bandari ya sehemu ya abiria kumekuwepo na harakati za ujenzi katika maeneo tofauti eneo la kwanza ni katika Tishali la Abiria ambayo tayari limekuwa kipaa pamoja na gazi kwa ajili ya kuwakinga abiria wetu kwa ajili ya kupata jua na mvua. Eneo la pili ni ujenzi wa vyoo vya abiria ubavuni mwa Taasisi ya Sayansi ya Baharini ambapo vyoo vinavyotumika hivi sasa vitabomolewa.

   Sehemu ya tatu ni kulifanyia matengenezo eneo linalotumika hivi sasa kupumzikia abiria pamoja na kuliengeza ukubwa.

   Aidha jengo la shirika lilokuwa karakana ya Maboya litafanyiwa ukarabati mkubwa bila ya kubadilishwa sura yake kwa ajili ya abiria na hakutakuwa na ujenzi mpya wa banda. Hilo la Ramp kwa ajili ya kufunga Vyombo vya aina ya *raw on- raw off* na *Landing Craft* nayo itaimarishwa kwa lengo la kurefushwa. Uongozi wa Shirika umekubali matengenezo hayo kufanywa na kampuni ya *Azam Marine* ambayo ndio iliyoomba kufanya matengenezo hayo kwa gharama zake mwenyewe na kwa masharti kuwa sehemu hiyo itabaki kuwa mali ya Shirika na itatumiwa na vyombo vyote vya abiria. Mabadiliko hayo yote yamefanywa kwa kufuata na kusimamiwa chini ya sheria ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe wa Zanzibar.

   (b) Jengo aliloomba kwa ajili ya matengenezo ya sehemu ya abiria halitatengenezwa mpaka hapo Mamlaka ya Uendeshaji wa Mji Mkongwe itakapotoa kibali cha ujenzi ingawa hivi sasa tayari mfadhili huyo ameshapeleka maombi na kusubiri majibu kutoka katika taasisi husika.

(c) Kampuni ya Bakhresa (*Azam Marine*) iliwasilisha maombi yake ya kutoa msaada huo kama walivyo wafadhili wengine kwa shirika letu na shirika liliyakubali maombi hayo baada ya kupitia katika ngazi uongozi wa Shirika uliyajadili maombi hayo na kuyakubali, kwa masharti ya kuwa eneo hilo halitakuwa kwa matumizi ya vyombo vya Kampuni yake tu bali litatumiwa na Kampuni zote zitakazohitaji huduma za eneo hilo. Aidha eneo hilo litamilikiwa na kuendeshwa na usimamizi na uongozi wa Shirika la Bandari la Zanzibar.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri.

Kwa kuwa eneo hilo ni mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na serikali sikivu, kikawaida inapotolewa zabuni, jee kuna zabuni iliyotangazwa kwa mujibu wa sheria ya mapinduzi inayotueleza katika mali za serikali.

Pili, pamoja na eneo hilo kutumiwa na Kampuni zote jee itakuwa ni haki mtu yeyote kufungua biashara pale au hatoruhusiwa mtu yeyote kufanya biashara na kama itakuwa ni haki nipate kuleta maombi kuja kufungua japo mkahawa mdogo mimi pale.

Tatu, Mhe. Naibu Spika, kwa kushuhudia na hansard zipo umekuwa mkali sana katika Baraza lako hili au Baraza lako hili ukisema Mji Mkongwe, leo Mji Mkongwe sijui haupo ulikwenda likizo kuvunja mabanda mule ndani bila ya mpangilio na banda limevunjwa pale na cha kusikitisha serikali hii kupata hasara pale kulikuwa pana *ramp* limejengwa kwa gharama chungu nzima ili meli zifunge na leo limevunjwa pesa zile leo zingesaidia serikali Wizara ya Afya kupata matibabu kule.

Sasa ninataka unieleze kwa makini Mhe. Naibu Waziri jee Mji Mkongwe haupo hata mabanda yale yakavunjwa au kuna sheria iliyopitishwa pale kuwa hapa wafanye hivi na wengine wasifanye.

Maana yake ulipiga kelele suala la magari kupita Mji Mkongwe itakuwa tunauchafua Mji Mkongwe. Mhe. Naibu Waziri ndio hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika…,

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa sikiliza jawabu zako halafu ndio utaondoka.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake matatu ya nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, tumeeleza katika jibu la msingi kwamba Kampuni ya *Azam Marine* ilileta maombi kwetu kama zinavyofanya mashirika na wahisani wengine. Sisi kama shirika tulichokifanya ni kuzingatia maombi yale tukayapatia katika uongozi wetu na tukaona kwamba maombi yale hayana tatizo. Msingi wetu ni kuona kwamba msaada utauendeleza uongozi na matumizi ya huduma ile kwa wananchi wote bila ya kuelekeza maeneo maalum au watu maalum, kwa maana ya kwamba msingi wa yule mtu ambaye ameonesha ule ufadhili.

Kwa hivyo hakukuwa na haja ya kufanya zabuni kwa sababu hatuwezi kufanya zabuni kwa msaada ambao tumeupokea. Tungefanya zabuni kama ingekuwa serikali ndio inaingia gharama ya kuendesha mradi ule.

Lakini jambo la pili ameuliza Mhe. Mwakilishi kwamba suala la uhuru watu kufanya biashara. Naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba eneo lile pamoja na kwamba linajengwa na Kampuni ya Azam Marine litaendelea kusimamiwa na kuendeshwa na Shirika letu la Bandari. Hivyo utaratibu wa mtu kufanya biashara kwa maana ya vyombo kuegesha na kupata huduma nyengine zitaendelea kama kawaida bila ya kujali ya kutambua kwamba *Azam Marine* ndiye aliyefadhili.

Jambo la tatu alilozungumza Mhe. Mwakilishi ni suala la Mji Mkongwe ni kweli kwamba mimi kama sehemu ya serikali tutaendelea kusimamia sheria zetu kuona kwamba wananchi wanazifuata na kuzitii na tumeeleza katika

majibu yetu kwamba mabadiliko haya yote yaliyofanywa yamefanywa baada ya kusimamiwa na kupitishwa na vibali na wahusika wa Wasimamizi wa Mji Mkongwe.

Tumeeleza kwamba maeneo ya mabanda ambayo bado hayajavunjwa lakini tuna azma ya kuyavunja na kufanya mabadiliko tumesita kufanya hivyo kwa kutambua kwamba bado kibali cha Mji Mkongwe hakijapatikana.

Lakini suala la kurefusha *ramp* ilikuwa ni miongoni mwa jitihada ya serikali ya kuona kwamba huduma hizi zinaimarika. Sasa kurefusha ramp, mimi naomba tu Mhe. Mwakilishi atupongeze sisi pamoja na huyo mshirika wetu wa maendeleo kwa maana ya kufikia maamuzi ya kuirefusha *ramp* ile ili kuimarisha huduma kwa vyombo vyetu vinavyoegesha katika maeneo hayo kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja dogo tu la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi kifupi tu hapa Mhe. Naibu Waziri hapa alikuwa akitujibu kwa hamasa kubwa sana katika namna ya kuziondosha meli za Jitihada katika pwani ya Forodha Mchanga na kuzihamishia katika eneo ambalo linategemewa kufanyiwa matengenezo ya banda la abiria.

Ninataka nimuulize ile azma ya mwanzo ya kuhamishia eneo lile kuleta M.V Jitihada pale limemalizikia wapi.

Lakini la pili, naomba anisaidie ni gharama za kiasi gani ambazo serikali hii zilitumika kujenga eneo lile ambalo linategemewa kuhamishiwa M.V Jitihada kutoka Forodha Mchanga kuja pale.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, samahani ameomba Mhe. Mwakilishi azungumze kwa taratibu mimi ninamsikiliza yeye asiye na haraka ninataka nimuelewe vizuri.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa uliza taratibu yeye yupo kwa ajili yako wewe usiwe na haraka.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ninataka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kwa kipindi kirefu alikuwa analizungumzia suala la kuhamishiwa meli ya Jitihada ambayo inapakia magari Forodha Mchanga kuhamishiwa kuja eneo ambalo hivi sasa ndio linajengwa kwa ajili ya jengo la abiria.

Shirika la Bandari limetumia gharama kubwa sana kujenga eneo lile, nataka kujua ule mpango umemalizikia wapi wa kuhamisha zile meli ambazo zilizokuwa zinapakia magari kule kuja hapa katika hili eneo.

La pili nataka nijue ni gharama za kiasi gani ambazo zimetumika kujenga eneo lile.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri umemfahamu sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Nimemfahamu. Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, azma ya serikali ni kuondoa huduma za *land craft* katika eneo la Forodha Mchanga kwa msingi kwamba la kwanza ni kusimamia na kuitekeleza sheria yetu ya uhifadhi wa Mji Mkongwe ya kutokuruhusu magari makubwa kuingia katika eneo la Mji Mkongwe.

Lakini jambo la pili masuala mengine yakiwemo ya kodi, taratibu za Forodha ya kwamba zinakiukwa na magari yanapitishwa kiholela. Sasa katika kutimiza azma hii, serikali kwa kushirikiana na huyu mfadhili ambaye tumemtaja, tumekuwa na *ramp* eneo la bandarini pale, *ramp* ile ikaonekana ni fupi na itakuwa ni usumbufu kwa vyombo kuweza kufunga.

Kwa hivyo tulichoweza kushirikiana kama uongozi wa bandari na wizara ni kwamba tumekubaliana kuwa ramp ile inarefushwa ili kuweza kuwa-*acommodate* hao watumizi wa meli watakaokuwa wanakuja kwa ajili ya kufunga.

Kwa hivyo kama kuna suala la gharama tumeshirikiana na huyo mfadhili katika kurefusha ramp iliopo ili kuondoa watu kutoka kule Forodha Mchanga kuja kufunga katika eneo la bandari.

Sasa madhumuni ya kufanya hivyo ni kuimarisha huduma kwa wananchi wetu lakini kutimiza ile azma ya serikali ya kuwaondosha wafanyabiashara na watumiaji wengine katika eneo la Forodha Mchanga kuja katika eneo ambalo litakuwa lipo vizuri na salama zaidi kwa ajili ya kutoa huduma za usafiri wa vyombo vya *raw on- raw off* na *land craft.*

Mhe. Omar Ali Shehe: Ninashukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza lenye sehemu (a), (b) na (c).

Mhe. Naibu Spika, katika jibu lake la msingi umekubali kwamba sehemu ile imefeli na hivi sasa imepewa Kampuni ya *Azam Marine* kwa ajili ya kuendeshea shughuli zake. Mhe. Ali kama nitakuwa sikosei alizungumza ni kiasi gani ambacho shirika kilitumia kwa ajili ya kujenga ramp ile ambayo sasa ambayo tunasema kuwa imefeli.

Ni kiasi ambacho shirika imetumia kwa ajili ya kujenga *ramp* na kwa kuwa *ramp* ile sasa imefeli na sasa sehemu ile atapewa mfanyabiashara, kwa nini shirika halikufikiria kudai gharama ile kwa yule mtu ambaye walimpa kujenga sehemu yake sasa. Kwa nini shirika halikuingiza katika mkataba kwamba fedha iliyotumika ile basi iwe ni sehemu ya fidia kwa shirika.

Lakini swali la (c) Mhe. Naibu Waziri huoni kuwa shirika kuamua kufanya mambo kwa kukurupuka na hivyo kupoteza fedha, huoni kuwa ndio sababu inayozifanya moja katika sababu inayofanya shirika kuendelea kuwa haliendelei mbele linarudi nyuma.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake matatu ya nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, suala la gharama halisi iliyotumika katika ujenzi wa mara ya kwanza ya ramp, naomba Mhe. Mwakilishi anikubalie nimletee kwa maandishi baada ya kwenda kuyachukua kutoka kwa watendaji wetu.

Lakini swali la pili ninapenda niweke *Hansard* vizuri. Mhe. Naibu Spika, hatukueleza kwamba eneo la *ramp* amepewa Kampuni ya *Azam Marine*, tulichokieleza kwamba eneo la *ramp* shirika linashirikiana na Kampuni ya *Azam Marine* katika kuirefusha, yeye ni mshirika na yeye ni mfadhili wa kusaidia kuirefusha *ramp* kwa ajili ya kuimarisha huduma.

Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Mwakilishi afahamu vizuri kwamba serikali na shirika hatujatoa eneo la bandari kwa kampuni binafsi. Yeye kama kampuni ni mshirika wetu wa maendeleo amekuja katika serikali na shirika kuja kusaidiana na sisi katika kurefusha eneo la ramp ili kuweza kuwa-commodate watumiaji wengine kwa ajili ya huduma ya meli za *raw on- raw off* na *land craft.*

Lakini la tatu ninamthibitishia Mhe. Mwakilishi kwamba shirika letu halifanya kukurupuka katika maamuzi yake. Walifanya tathmini ya kina, wakafanya maamuzi wakajenga.

Kama sote tunavyofahamu Shirika la Bandari hasa eneo la gati pale kuna tatizo kubwa sana ambalo limejitokeza pengine wengi miongoni mwetu hatulifahamu. Kuna tatizo hivi sasa la bandari kudidimia kwa maana ya kwamba kile kima au wingi wa mchanga unaongezeka na kima cha maji kinapungua, pengine tungewaachia wataalamu wakaendelea na utafiti, wakaja kutwambia kitu kulichotokezea hatimaye tukaja tukafikia maamuzi.

Nadhani Mhe. Naibu Spika, si sahihi kwetu sisi wana siasa tukafikia maamuzi ya moja kwa moja katika maeneo yanayohusu utaalamu, jambo ambalo ninadhani tungewapa nafasi watu wetu wataalamu wakaendelea na uchunguzi na baadae majibu yao tukaja tukayafikisha katika vyombo husika.

Nam. 24

Serikali Kushindwa Kuuendeleza Mchezo wa Riadha Zanzibar

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza**:-**

Mhe. Naibu Spika, katika miaka ya mwanzoni mwa thamanini (80's) Zanzibar iling'ara katika medani ya mchezo wa Riadha. Na kwakuwa mafanikio hayo yalipatikana baada ya Serikali kuchukuwa juhudi ya kuupeleka mchezo huo Maskulini pamoja na kuajiri kocha wa kigeni kutoka nje ya nchi.

Je, kwanini Serikali imeshindwa kuuendeleza mchezo huo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 24 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Wizara inasimamia vyama thalathini (30) kikiwemo Chama cha Riadha na vyama vyote vinahaki sawa katika kuviendeleza. Serikali bado haijashindwa kuendeleza mchezo wa Riadha, kwani mchezo wa Riadha umekuwa ukishiriki mashindano mbali mbali pamoja na makombe. Na katika kuthibitisha hili safari nyingi ambazo zinafanywa na Chama cha Riadha zinagharamiwa na Wizara yangu, kupitia Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar.

Kwa mfano mashindano yaliyofanyika Botswana na mashindano ya *Senior East Champion Ship* yaliyofanyika Dar-es-Salaam. Vile vile hivi karibuni tu tarehe 13/09/2012 Chama hicho kilikwenda katika mashindano ya Taifa 'Tanzania National Championship" na washindi walikuwa ni chama cha Riadha cha Zanzibar kwa wanaume na wanawake pia ushindi wa jumla.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza lenye kipengele (a) na (b).

a) Kwa kuwa katika *football* Zanzibar hatufanyi vizuri na kwa kuwa katika swali lanngu la mwingi nilisema kwamba katika miaka ya 1980 Zanzibar kulikuwa na ustaarabu wa kuagiza makocha kutoka nje na makocha wa riadha na hata wa football alikuja Tambwe leya, yule wa riadha jina lake limenitoka. Jee, ni lini Zanzibar itaagiza kocha wa kimataifa ili tuweze kufanya vizuri katika medani kama vile olympic kama sio michezo ya *CECAFA*, olympic ndio ninayozungumzia kama tulivyofanya katika miaka ya 1980 tuliwahi kuleta medali ya dhahabu hapa. Jee, lini mutafikiria kuimarisha riadha kwa kuleta kocha wa kimataifa kuweza kufundisha hapa na hatimaye kuleta tija medali za dhahabu katika olympic. Hilo la kwanza.

b) Kwa kuwa Chuo cha Ualimu hapa Nkrumah ambapo hivi sasa ni tawi la *SUZA* ile, katika miaka 1980 walianzisha kozii moja makini sana walikuwa wanaita kozi ya Diploma in Physical Education, wakatoa wataalamu wazuri sana katika mambo haya physical education, michezo hii mambo ya fani art tukamtoa mpaka kocha Suleimain Mahmoud (Sule) kwa kupitia diploma ile pale ya phycal education, wapo wataalamu hao wazalendo wenye uwezo mkubwa katika mambo ya riadhaa. Jee, wizara yako kupitia Idara ya Michezo munawatumia wataalamu hawa katika kuendeleza medali hii ya riadhaa kwenye nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

a) Mhe. Naibu Spika, ninakubaliana na Mhe. Mwakilishi sasa hivi Chama cha Riadhaa kina uchaguzi na kitakapofanya uchaguzi wake kama ipo haja ya kutushirikisha wizara, itakapopata viongozi wake tutakaa ili tuwapate wataalamu wa nje au wataalamu wazalendo.

b) Mhe. Naibu Spika, ni kweli hayo yote anayoyasema lakini tupo pamoja na vyama hivyo kwa kushirikiana na wizara ili kuendeleza walimu hao ili serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na vyama vyetu vya michezo vipate ufanisi wa hali ya juu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii nikamuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo tu la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza ninataka nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa jinsi alivyolijibu swali zito la Mhe.Salah kwa ufasaha mkubwa.

Sasa swali langu Mhe. Naibu Spika, nataka nimuulize Mhe. Naibu Waziri kama hivi ifuatavyo.

Kwanza tunawashukuru sana wana riadhaa wetu wa Zanzibar kwa kushirikiana katika mashindano yaliyofanyika hivi karibuni kule Tanzania Bara na wakaweza kurudi na kupata ushindi mkubwa. Lakini Mhe. Naibu Spika, kwamba wana riadhaa wetu hivi sasa wamekuwa wakijitahidi sana na Zanzibar tuna vipaji vya wana riadhaa, lakini bado inaonekana huduma kwa wana riadhaa hawa zinakuwa hafifu.

Mfano hata haya mashindano waliyoshiriki hivi karibuni huko Tanzania Bara basi hata nauli walikuwa wanahangaika hangaika. Sasa jee, swali langu lipo hapa.

Jee, wizara kuwapa moyo vijana hawa wanaoshiriki riadhaa na kwa kuwa wana uduni wa vitendea kazi hasa vifaa vya kufanyia mazoezi. Wizara ina mpango gani wa kuweza kuwatafutia wadhamini alau wa kuweza kuwasaidia vifaa na gharama za maandalizi ya michezo.

Lakini swali la pili Mhe. Naibu Spika, wizara wakati mwengine kwamba ina ukwasi au haina kitu cha kuweza kuwasaidia wakati mwengine. Lakini jee baada ya kurudi katika michezo hiyo kule Tanzania Bara na wakapata ushindi mkubwa kabisa na medali nyingi tu wamerudi nazo, basi wizara hata kuwaita na kuwapongeza na kuwapa ahsante pia hili linahitaji gharama gani. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kuniruhusu kujibu swali la nyongeza la Mhe. Hamza Hassan Juma.

Kwanza kwamba ni kweli Mhe. Naibu Spika, vijana hawa wa riadhaa wanafanya kazi nzuri katika mazingira magumu, na serikali kupitia wizara yangu imekuwa wakati wowote ipo na vijana hawa kuona kwamba jitihada zao angalau tunawapa moyo.

Jambo moja kubwa ambalo limekuwa likiwakwaza muda mrefu ni kwamba walikuwa hawana uongozi, hili lilikuwa ni tatizo kubwa uongozi wa kudumu na wizara ilikuwa ikishikiriana nao hao viongozi wa muda kuona kwamba wanapata uongozi taasisi iliyokamilika kuendeleza michezo.

Nina furaha kuwa kwamba jitihada hizo zipo katika hatua ya mwisho na pia kwamba nimesikia kuwa hata baadhi ya Wajumbe wa Baraza lako Tukufu Mhe. Naibu Spika, ni miongoni mwa watu wanagombania uongozi katika chama hicho, mimi binafsi limenipa moyo kwamba hata ndani ya Baraza nitakuwa na watu wa kushirikiana nao katika kuendeleza mbele mchezo huu wa riadhaa kwenye nchi yetu. Kwa hivyo hilo ni jambo zuri ambalo linapaswa kushukuriwa.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba jitihada hizi zitakapofanikiwa za kupata uongozi wizara yangu itashirikiana na uongozi huo kuhakikisha kwamba yale yote ambayo hivi sasa yanawasumbua katika kuendeleza mbele mchezo huu basi tunashirikiana kwa karibu.

Tumepanga kwamba baada ya uongozi huo kukamilika tutawaita kwa pamoja ili kupanga mikakati ya namna gani kwa pamoja katika kuwatafutia wadhamini na pia katika kuhakikisha kwamba mambo madogo madogo ambayo yanawasumbua basi yanapatiwa ufumbuzi ili kuendeleza mbele mchezo huu wa riadha hapa Zanzibar.

Nam. 11

Kutoajiriwa kwa Vijana Waliomaliza Masomo ya Sayansi

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kwa kuwa Zanzíbar tuna tatizola kudumu la walimu wa masomo ya sayansi katika skuli zote za Unguja na Pemba na kwa kuwa Chuo cha Kiislamu katika muhula wa mwaka 2011/2012 tayari wametoa walimu wa stashahada (Diploma) za sayansi na hadi leo hii baadhi yao hawajaajiriwa.

Jee, ni sababu gani za msingi zilizopelekea wahitimu hao adimu wasiajiriwe.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri subiri kidogo kwa kuwa muda wa maswali unakaribia kumalizika na tumebakia na swali moja, tunamuomba Mhe. Waziri aje atoe hoja ya kuongeza muda.

KUONGEZWA MUDA WA MASWALI

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda uliopangwa kwa ajili ya maswali unakaribia kumalizika, na kwa sababu bado kuna swali moja la kujibiwa, naomba Baraza lako litengue kanuni ya muda kuhusiana na maswali, ili tumalize kujibu swali lililobakia ili tuendelee na hoja nyengine zilizobakia. Naomba kutoa hoja Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale waliokubaliana na hoja. Waliokataa. Waliokubali wameshinda. Waziri tuendelee, endelea kujibu swali.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza naomba kumtakia safari njema ya Hijja Naibu Waziri wangu ambaye aliondoka jana usiku, na ndio maana leo niko hapa kujibu haya maswali

Mhe. Naibu Spika, ni kweli skuli zetu nyingi za sekondari zina upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi. Ni kweli kuwa Chuo cha Kiislamu katika mwaka 2011/2012 kilikuwa na wahitimu wa diploma ya walimu wa sayansi. Kwa kupunguza uhaba wa walimu wa sayansi waliopo, wizara katika mwaka 2011/2012 iliajiri jumla ya walimu 104, ili wasomeshe katika skuli zetu sa sekondari masomo hayo ya sayansi. Walimu hao waligaiwa kwa Unguja na Pemba katika skuli zetu za sekondari.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013 wizara yangu imekusudia na imeshapeleka maombi ya kuajiri walimu 1,000 wa sayansi, ili iwapeleke skuli mbali mbali kupunguza tatizo la upungufu wa walimu hao. Ombi hili limeshapelekwa Tume ya Utumishi Serikalini, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ili kupatiwa kibali au ruhusa ya ajira hizo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniruhusu kuuliza swali moja la nyongeza. Lakini kabla ya hapo niungane na Mhe. Waziri kwa kuendelea kumtakia Naibu Waziri wake wa Elimu, safari njema na yenye maslahi ya Hijja. Mwenyezi Mungu ampeleke salama na amrudishe salama. Baada ya hayo naomba kuuliza swali dogo la nyongeza, lenye kipengele (a) na (b).

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba nafasi 1,000 za walimu wa sayansi zimeshatangazwa. Je, ikiwa serikali itakubali kuwaajiri hawa walimu 1,000 wa sayansi, je kutakuwa na ulazima tena wa kwenda Nigeria kwenda kuwachukua Wanigeria kuja kutusomesha sayansi hapa. Hilo swali (a).

(b) Kwa kuwa vyuo vyetu vikuu hapa Zanzibar yaani *SUZA*, Tunguu, Chukwani kuna walimu wengi tu wenye taaluma ya sayansi na wanaweza kusomesha *ordinary level* na *advance level*. Je, serikali ina mpango gani madhubuti wa kuwanasihi wataalamu hawa kuingia nao mkataba wa kusomesha *part time* katika skuli zetu za serikali na hatimaye kunusurika na kuwaleta Wanigeria katika visiwa hivi. Hapo sasa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mjumbe ameuliza baada ya kuajiri hao walimu 1,000 je kutakuwa na haja tena ya kuagiza walimu kutoka Nigeria. Jibu ni kwamba walimu 1,000 tutakaowaajiri wamo wa sayansi na masomo mengine. Hata ingekuwa wote 1,000 ni walimu wa sayansi, bado utaratibu wetu wa kuajiri walimu kutoka Nigeria, Pakistani, India na Misri bado ungekuwa unaendelea kwa sababu tunahitaji walimu wengi wa sayansi wenye uwezo mkubwa. Kwa hivyo, nitalijibu vizuri swali hili wakati nitakapojibu kuna swali huku linazungumzia uajiri wa walimu kutoka Nigeria.

Mhe. Naibu Spika, walimu wa sayansi waliostaafu, kama kuna uwezo wa kuwashawishi tukawaajiri tena hawa kwa mikataba. Mhe. Naibu Spika, katika walimu wa sayansi waliostaafu, bila shaka hawa ni watu wazima, wameshafikia miaka zaidi ya 60, kwa wale wanaojiweza kiafya basi tunawashawishi, lakini wengi wao wanakataa na wanasema sasa wakati wa kupumzika umeshafika.

Kwa mfano, kulikuwa na mwalimu mmoja mzuri sana wa sayansi alikuwa anasomesha Haile Sellasie, huyu sio kumshawishi tu, tumembembeleza arudi tutamlipa vizuri atusome wanafunzi wetu angalau kwa miaka miwili tu, huyu mwalimu amekataa. Kwa hivyo, tunajitahidi na tunajaribu lakini mwalimu akishafika kustaafu baada ya kazi kubwa sana ya kusomesha, basi hupenda sasa apumzike. Lakini ushauri wake tunauchukua, jitihada zetu tunaziendeleza na atakayekubali tutampokea kwa mikono miwili.

Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Mjumbe kama yeye anaye mwalimu kama mmoja au wawili, watatu au wanne anaweza kutusaidia kuwashawishi basi atuletee tutawapokea. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kama hivi ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa jitihada kubwa ambayo tangu kukabidhiwa hii wizara ameanza kuionesha hasa katika suala zima la kuwaajiri walimu ili kuweza kuondoa tatizo la walimu hapa visiwani kwetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri ameelezea ni namna gani anavyofanya jitihada za kuwabembeleza walimu wastaafu wa sayansi kurudi tena kuja kuwasomesha vijana wetu, angalau kuweza kuwapatia ile taaluma ambayo inastahiki. Lakini bado kuna wengi wao kama alivyosema wamepitwa na umri, lakini wengine wanasema kutokana na afya hawawezi tena kuendelea.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, swali langu liko hapa. Hivi sasa kuna wanafunzi wa sayansi ambao wameomba mkopo wa elimu ya juu, ili kwenda kusomea hizo fani za sayansi ili wakirudi waje waweze kushika nafasi za wale waliostaafu. Lakini bado wizara inakuwa na ugumu wa kuweza kuwapa mikopo ya elimu ya juu hawa wanafunzi kwa ajili ya kujenga hao wataalamu wa baadae kuja kuwasomesha hawa vijana wetu. Sasa je Mhe. Waziri haoni upo umuhimu katika hii mikopo yetu ya elimu ya juu, bado wale wanafunzi wanaoomba mikopo kwa ajili ya kusoma masomo ya sayansi serikali kuweza kuwapa kipaumbele ili hili tatizo la upungufu wa walimu wa sayansi liondoke hapo baadae. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwanza nazipokea pongezi zake za kunipongeza kwa kazi nzuri tunayoifanya katika wizara, ili iweze kusaidia kuiendeleza wizara yetu.

Pili amezungumza kuhusu walimu wastaafu na kama nilivyotangulia kumjibu Mheshimiwa mkereketwa Mhe. Saleh Nassor Juma Mwakilishi wa Jimbo la Wawi, kwamba tunajitahidi na kwa mujibu wa walimu hao waliostaafu kwa uzoefu wao na ujuzi wao, basi tungependa tuwe nao, maana aghalabu ruhusa ya kuajiri kwa mkataba mwaka mmoja na miaka miwili inaruhusiwa, seuze hawa walimu ambao tuna upungufu nao mkubwa sana wa sayansi.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Hamza Hassan Juma kama kawaida yake ya kushirikiana na mimi na Wawakilishi wengine, katika jimbo lake kama wapo au katika eneo jengine anawajua wapo, tusaidiane. Tuwashawishi, ili tuwape mikataba ya miaka miwili ili watusaidie kusomesha.

Swali la mwisho ni kwamba wapo walimu wenye diploma ya sayansi, wameomba mikopo ili waweze kujiendeleza na bado mikopo yao hawajafanikiwa hatujawapa mikopo, hivyo anashauri hawa tuwape kipaumbele.

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana sana na Mhe. Hamza Hassan Juma na ndivyo tulivyofanya mwaka huu. Tumeweza kuwapa mikopo baadhi ya walimu wetu wenye Stashahada kwenda kusoma digirii ya mwanzo kwa masomo ya sayansi.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumuahidi kwa mwaka ujao tutawapa kipaumbele zaidi, kwa sababu hawa hata tukiwakopesha, wana uwezo wa kulipa kwa sababu ni walimu wetu, sioni tatizo hata kidogo kwa nini tusiwakopeshe. Ila tatizo mwaka huu, kama nilivyowahi kueleza nilipokuwa nikijibu swali hili zamani kidogo, kwamba pesa tulizonazo bado ni kidogo hazitoshi, ingawa tumeongezwa mara mbili zaidi ya *estimate* ya mwaka jana, lakini bado tuna madeni ya wanafunzi wengi walioko masomoni, wa mwaka juzi, mwaka jana na kabla ya

hapo na malipo ya waliokopa bado yanakwenda pole pole ingawa bado tunayapata, lakini yanakwenda pole pole hatukuweza kuwaweka waombaji wengi zaidi kuliko wale tuliowaongeza. Lakini waombaji wa mwaka huu, tumewapata mara mbili zaidi kuliko wale tuliowapata mwaka jana. Kwa hivyo, juhudi zinaendelea, pesa tunazo tunatiliwa ingawa kidogo, lakini bado juhudi zinaendelea na tutaziendeleza mpaka tuhakikishe jambo hili limekamilika. Ahsante sana.

Nam. 12

Kutolipwa Haki zao Walimu Wanaomaliza Mafunzo ya *TAP*

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kumekuwa na tatizo la kudumu la walimu waliomaliza mafunzo yao ya (*TAP*), *Teachers Advance Programe*, kutolipwa mafao yao baada ya kumaliza kozi hiyo; na kwa kuwa serikali mara kadhaa inatoa ahadi ya kuwalipa walimu hao, lakini hadi leo hii bado hawajalipwa.

(a) Je, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kuwa kuendelea kufanya hivyo ni kuwadhulumu walimu hao.

(b) Kwa kuwa wanachodai walimu hao ni haki yao, na kwa kuwa haki na wajibu vinaenda sambamba; Je, serikali haitawachukulia hatua walimu hao pale watakapovunjika moyo na kurudi nyuma katika kuwatumikia wananchi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 12 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, walimu waliohudhuria masomo ya *Teachers Advance Programe*, yaani *TAP*, ni walimu waliomaliza Stashahada ya Diploma na kupangiwa kusomesha sekondari mbali mbali kwa Unguja na Pemba. Walimu hao wako makusudi na walipangiwa kushiriki katika programu hizi za *TAP* kwa kipindi cha miaka miwili, kwa mahudhurio ya siku moja kwa wiki ili kuwaendeleza katika taaluma yao ya sayansi.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kabisa walimu hawa wa sekondari wanasomesha huko vizuri na wanatusaidia. Lakini ni kweli pia kwamba bado mishahara yao au nyongeza ya mishahara yao hatujawapa.

Mhe. Naibu Spika, hatua tayari zimeshakamilika za kuwapa nyongeza zao na maombi yameshapelekwa Idara ya Utumishi, ili watupe kibali cha kufanya hivyo. Baada ya maelezo hayo, naomba sasa kumjibu swali lake nambari 12 lenye vifungu (a) na (b).

(a) Mhe. Naibu Spika, hatuna dhamira hiyo wala hatutokuwa na dhamira hiyo ya kuwadhulumu walimu hawa. Walimu hawa ni wetu, tumewasomesha, wanajitihada na kwa nini tuwadhulumu. Kama nilivyosema mipango ya kuwapa stahiki zao na mishahara yao inayostahiki imeshakamilika. Tulikuwa tunasubiri bajeti na bajeti imeshakuja, fedha tunazo na tumeshaziomba, mara tu tukipata kibali cha kuongezea mishahara yao na kuwapangia mishahara yao mipya na maposho, basi tutafanya hivyo.

(b) Mhe. Naibu Spika, swali lake anauliza walimu hawa wakivunjika moyo, wakigoma na mengineyo je, serikali itawahukumu. Mhe. Naibu Spika, naomba walimu hawa hawakusikia hivi Mhe. Nassor alivyozungumza. Kwa hivyo, hawatogoma, hawatokataa na wataendelea, na ninawaomba sana waendelee kuwasomesha vijana wetu kwa juhudi zao kubwa kama wanavyofanya sasa. Ninawaomba wanisikie kwamba mishahara yao tumeshawatengenezea pamoja na maposho yao, mara tu tukipata kibali cha Idara ya Utumishi watafurahi. Ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza niendelee kumkumbusha jina langu kamili Mhe. Waziri. Jina langu ni Saleh Nassor Juma Mwakilishi wa Jimbo la Wawi ni miongoni mwa *Twayyibul Asmai Wahibru Umma* pale Wawi. Baada ya utambulisho huo naomba niulize swali dogo la nyongeza lenye vipengele (a) na (b).

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa haki ikichelewa kutolewa ni sawa na kwamba haikutolewa kabisa. *Justice delayed is justice denied,* na kwa kuwa haki haiwezi kupatikana katika kisahani cha chai kama vile halua tu au tende ni lazima idaiwe, na kwa kuwa ng'ombe akivunjika mguu malishoni hujikokotea zizini kusaidiwa, na kwa sababu hili jibu la leo, kesho na keshokutwa watapata haki zao, utumishi wameshaomba huu ni mwaka wa nne walimu hawa bado hawajapata haki zao.

(a) Je, Mhe. Naibu Spika, sitoeleweka msaliti pale nitakapoongozana na jopo la walimu hawa kuelekea zizini kwa maana ya Ikulu kwenda kwa Mhe. Rais kudai haki hizi.

(b) Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ataje siku ni lini walimu hawa watalipwa ili labda tuache hiyo safari ya kwenda kwa Rais kuomba haki hiyo. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma, Swahibu yangu wa Jimbo la Wawi, mkereketwa mwenzangu, swali lake la nyongeza. *(Vicheko/Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, huu usemi mimi naukubali, haki ikicheleweshwa ni sawa sawa na haki kukataliwa. Lakini usemi huu unaambatana na haki kucheleweshwa kijanja janja, sio haki kucheleweshwa kwa sababu. Sababu nilizozieleza Mheshimiwa natumai sana umezifahamu na natumai sana kuna siku ulilizungumza hili kwenye Kamati na ukasema katika hali hii, haki zinacheleweshwa kama hivi kwa sababu pesa hatupati. Sasa leo naona kidogo umekuwa mkali na umezungumza kwa lugha tofauti. *(Makofi).*

Bado nakuomba Mhe. Mjumbe ukubaliane na mimi kwamba juhudi za kuzitafuta pesa hizi tunazichukua. Tumezipeleka katika bajeti, bajeti imekubaliwa, lakini pesa hazijaingizwa. Nataka nikuambie kwamba katika kipindi tokea tumeanza bajeti mpaka sasa hivi, wizara yangu imeingiziwa shilingi 300,000,000/= kwa ajili ya kumaliza SUZA ilioko Tunguu, ili watu wapate kuhamia kwa haraka. Bado mpaka sasa hivi hatujapata pesa nyengine. Lakini ninategemea sana kwamba tutazipata pesa hizi hivi karibuni na haki hii iliyocheleweshwa itakamilishwa.

Lakini hili swali la pili la kusema muende kwa Rais mukaombe haki hii itekelezwe. Mimi nafikiri Rais keshanisikia nilivyozungumza. Sasa mimi sioni sababu ya kupeleka ujumbe au kwenda kwa Rais kwenda kudai haki hii, maana haki hii haijakataliwa. Nimesema mara mbili, na hii sasa nasema mara ya tatu kwamba haki hii ipo, sina dhamira ya kuwadhulumu walimu wangu. Nina dhamira ya kuwapenda sana walimu wangu na kuwasaidia sana walimu wangu, na pesa hizi watazipata punde si punde.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara Zanzibar ya Mwaka 2012

(Kusomwa Mara ya Pili)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kufanya majumuisho ya majadiliano ambayo Waheshimiwa Wajumbe waliyatoa.

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Kamati yako ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa michango yao yote ambayo mlitupa kuanzia mwanzo mpaka katika Baraza hili. Michango ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilikuwa ni mizuri na kutoka mwanzo ndio tuliyoifanyia kazi mpaka tukafikia kuwasilisha mswada huu katika hali iliyokuwa. Kwa hivyo, mimi binafsi na kwa niaba ya wizara na watendaji wenzangu tunawashukuru sana Kamati ya Katiba na Sheria.

Mhe. Naibu Spika, vile vile napenda niwashukuru Wajumbe wote waliochangia ambao ni 12, na michango yao kwa kweli imeonesha kwamba mswada huu wameufahamu vizuri

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mnaotoka nje, karibu Mhe. Waziri atamaliza tunataka tupitishe vifungu. Kwa hivyo, anayetoka arejee ndani haraka.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Kwa sababu wameufahamu vizuri, kwa kweli mimi nitakuwa sina majibu mengi ya kuwajibu, kwa sababu yale ambayo walikuwa wanachangia, ndio hasa yaliyotufanya kuuleta mswada huu ili tuweze kuyarekebisha hayo mambo ambayo waliyoyachangia. Hasa kwa mfano Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Hamza Hassan Juma ambayo yote waliyoyasema yale ndio hasa yaliyosababisha kuletwa mswada huu ili kuyarekebisha.

Lakini zaidi Mhe. Naibu Spika, napenda niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe hawa ambao walichangia. Kwanza ni:

1. Mhe. Wanu Hafidh Ameir kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
3. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
4. Mhe. Hamza Hassan Juma
5. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
6. Mhe. Mussa Ali Hassan
7. Mhe. Abdalla Mohamed Ali
8. Mhe. Marina Joel Thomas
9. Mhe. Fatma Mbarouk Said
10. Mhe. Asaa Othman Hamad
11. Mhe. Abdi Mossi Kombo
12. Mhe. Saleh Nassor Juma

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaenda katika hoja za mmoja mmoja. Naomba niseme mambo manne ambayo haya naamini kwamba yatajibu masuali ya takriban Wajumbe wengi ambao waliuzungumzia.

Kwanza ni kifungu cha 3 katika ufafanuzi. Waheshimiwa Wajumbe wengi walikuwa wanataka kujua, ile tafsiri ya maneno ya maana ya biashara binafsi, na tukasema maana yake ni chombo kisichojitegemea.

Mhe. Naibu Spika, hili lengo lake ni moja, kwa sababu kuna vyombo vya aina mbili. Kwa mfano, kama kampuni, lakini kuna biashara nyengine ambazo zinaitwa *partnership.* Sasa kampuni siku zote tunaposema, tunasema zile zina *legal status,* yaani unaweza ukaishtaki na inaweza ikashtakiwa au ikashtaki.

Lakini chombo hichi tulichokusudia ni *partnership* huwezi kukishtaki kile chombo chenyewe, lakini wale watu binafsi ndio unaoweza kuwashtaki. Kwa hivyo, hii ndio tofauti kubwa baina ya vyombo hivi, na ndio maana pale tukasema ni chombo kisichojitegemea.

Mhe. Naibu Spika, la pili napenda niseme tu kwamba baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe walichanganyisha mswada huu na mswada wa pili pengine tutausoma Jumatatu tukijaaliwa na hasa katika madhumuni na sababu.

Kwa kweli mwanzo nilisema hapa kwa bahati mbaya na niliomba radhi kwamba madhumuni na sababu ya mswada huu tunaouzungumza yalichanganyishwa na madhumuni na sababu ya mswada ule mwengine. Kwa mfano, suala la Mkurugenzi Mtendaji halimo katika mswada huu, lakini watu walilijadili.

Kwa hivyo, hiyo naomba tujue hivyo na kwamba yale yote ambayo yalikuwa hayamo katika mswada huu, basi tuyaache mpaka katika mswada mwengine unaofuata.
Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa na kuhusu kifungu cha 24, ambacho kilizungumzia juu ya uwekaji sawa taarifa, pale tulisema kwamba kwa zile kampuni ambazo zimeshasajiliwa tokea zamani basi sheria hii itawahusu pia. Lakini watachukuliwa kwamba na wao tayari wameshasajiliwa, isipokuwa wataendelea kwa kipindi cha mwaka mzima na baadaye ndio watatakiwa wajisajili rasmi.
Kwa nini tukasema hivi, kwa sababu mara nyingi kampuni zina utaratibu wake, ambapo huwa wanakutana au huwa na mkutano mkuu wa ile kampuni na mara nyingi huwa kila baada ya mwaka mmoja. Sasa tunapowapa nafasi ya mwaka mmoja, yaani tunawapa wao nafasi ya kukutana, ili waweze kuyajadili yale mambo ambayo yameelezewa katika sheria hii kwa ajili ya kuyatimiza na halafu tena baadaye waje kujisajili.

Mhe. Naibu Spika, suala la kujisajili kama walivyouliza baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe itakuwa ni bure, kwa sababu wao watakuwa tayari wameshajisajili tokea zamani.

Madhumuni makubwa ni kwamba tunataka tupate taarifa za kampuni zile ambazo tayari zimeshasajiliwa na pia kukusanya mambo kadhaa ambayo tayari yameshawahi kujitokeza katika maeneo mengine.

Jambo la tatu ambalo liliulizwa ni kwamba je kwa nini tunasajili kampuni katika sheria hii, wakati kuna sheria nyengine ambazo tayari zimeshasajili. Mhe. Naibu Spika, ni kweli lakini kama nilivyosema mwanzo wakati nilipokuwa nikielezea ni kwamba hizi kampuni zipo nyingi na kuwepo kwa kampuni nyingi katika sheria mbali mbali nayo imetuletea matatizo. Kwa mfano, utakuta kampuni ambazo zipo katika Sheria ya Kampuni, utakuta nyengine ziko katika jumuia, utakuta vyama vya ushirika na hivi vyote vina sheria tofauti.

Kwa hivyo, hizi zinaleta matatizo kwa sababu hatuwezi kuzijua ni kampuni ngapi tulizonazo na wala hatuwezi kujua mapato kiasi gani ambayo tunayapata. Sasa zote zikiwa zipo kwenye mwamvuli mmoja, basi naamini zinaweza kusaidia sana kusaidia pato la serikali.

Mhe. Naibu Spika, hii imeshawahi kutokewa na kuleta matatizo kwa baadhi ya kampuni ambazo zimesajiliwa mwahala tofauti. Kwa mfano, nakumbuka katika muda wa nyuma kidogo kulikuwa na kampuni mmoja iliyosajiliwa kwa jina la Ushirika wa Donge. Kwa hivyo, halafu kampuni ile ile ikasajili kwa namna au utaratibu mwengine kwa jina la Kiingereza na kusema *Donge Cooperative Society* kitu kama hivyo, kwa hivyo utaona hizi ni kampuni mbili lakini *infact* itakuwa ni kampuni moja.

Sasa walipopata fedha zile fedha zikatiwa katika *Donge Cooperative Society* kumbe vile zile zilikuwa zinakwenda kwa Ushirika wa Watu wa Donge na ikawa ni zogo kubwa sana. Kwa maana hiyo, yote haya ndio yanayosababisha at least zile kampuni zote zikiwa chini ya mrajis mmoja, basi zinaweza zikawa *monitored*, na katika utandawazi wa siku hizi unapozipeleka zile kampuni kama imeshasajiliwa basi ni rahisi kujua na kuweza kumwambia kwamba hii tayari imeshasajiliwa au bado. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tunaweza kupata au kufanya utaratibu mzuri wa kujua kampuni zote na kwa maana hiyo tukipata taarifa zao kwa pamoja na tukapata idadi ya zile kampuni, kwa sababu siku hizi kuna lile suala la *E-Government* ambalo linakuja, kwa hiyo hii itakuwa ni rahisi kuyadhibiti kampuni hizi.

Mhe. Naibu Spika, ukeshakuwa na pahala pamoja ambapo unayo ile orodha ya kampuni zote, kwa sababu ya mtandao hivi sasa ndio umo katika hatari, basi ni rahisi pia kuweza kuwabana hawa kulipa au kuhakikisha kwamba ushuru ama kodi zinazotakiwa zinalipwa ipasavyo.

Kwa mfano, unapokuja kusajili katika ofisi hii ya kampuni na kwa sababu ya mtandao, kwa hiyo watu wa kodi watajua pamoja na wengine pia watajua, basi mnaweza ku-*monitor* ili kudhibiti ule utaratibu mzima wa ulipaji kodi. Kwa maana hiyo, Mhe. Naibu Spika suala hili ni muhimu kulifanya lote chini ya sheria moja.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa ujumla niseme tu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wengi tukianza Mhe. Abdalla Juma Abdalla alizungumzia, je kuna haja gani ya kuwasajili katika sheria hii wakati kampuni hizi tayari zimeshasajiliwa.

Kwa kweli kama nilivyosema kwamba suala hasa ni kuziweka chini ya mwamvuli mmoja, ili kurahisisha mapato, kuunganishwa na kuona kwa sababu ukishasajili katika utaratibu mmoja, basi itakuwa kampuni ina namba yake. Kwa hivyo, namba yake ile kama wenzetu wanavyofanya basi popote utakapoipeleka wanaweza kujua siri au maelezo yote ya kampuni ile, je kama huyu ameshalipa kodi au bado, pia kama anayo matatizo au hana, kwa hiyo hii itasaidia katika nyanja hizo.

Mhe. Naibu Spika, jambo muhimu ni kusaidia kupata fedha ambazo hivi sasa kila mtu ana-*register* katika sheria mbali mbali ambazo zile hatuna *control* nazo. Hivyo, yote hiyo itapunguza urasimu wa aina hiyo.

Jambo la mwisho ambalo ni muhimu lengo hasa ni baadaye kufanya kampuni hizi au ule usajili wa kampuni zote ziwe chini ya mwamvuli mmoja, yaani *One Stop Centre*. Kwa hivyo, mtu anaweza kuja kwa urahisi na kufanya vitu vyake vyote anavyotakiwa pale pale. Kwa mfano, mtu akitaka kusajili kwa mtandao ataruhusiwa.

Vile vile kwa mfano wenzetu Burundi unaweza kusajili kwa mtandao na ikawa ni bure, lakini ukienda ofisini na kutaka kusajili pale lazima ulipe kwa sababu ya zile gharama ambazo wafanyakazi wanaingia. Mhe. Naibu Spika, haya ndio madhumuni makubwa.

Pili Mhe. Naibu Spika, ilielezwa kwamba je kampuni ikishasajiliwa au utaratibu gani ambao utafanywa kwa kampuni ambazo zina majina mawili na zikienda wakati mmoja wa kusajili. Kwa kweli mimi nafikiri kama tulivyoeleza katika sheria ni kwamba *first come* ndio *first served*.

Kwa hivyo, kama unakwenda na jina fulani na halafu mwenzako akija na jina fulani, basi yule aliyekwenda mwanzo ndiye ambaye atakayekuwa *registered* katika jina lile na mwengine ataambiwa atafute jina jengine. Mhe. Naibu Spika, hii itasaidia sana kupunguza haya mambo ya ubabaishaji.

Kwa mfano, hivi sasa kuna kampuni tumezigundua zina jina sawa na jina jengine, sasa unaweza kufanya shughuli zako kwa kampuni ile lakini zile shughuli zikawa ni mbaya na wala haziridhishi. Sasa yule na mwenzako anayo kampuni kama ile iliyofanana ambaye yeye *products* zake ni nzuri, lakini kwa sababu ya lile jina tu kwa hiyo na yeye akaathirika. Kwa maana hiyo, hii pia italeta ile *control* ya zile kampuni na itaweza kusimamia ubora wa utendaji kazi katika shughuli hizi.

Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na Mhe. Ismail Jussa Ladhu karibu maelezo yao yalikuwa yanafanana. Kwa hivyo, kama nilivyosema kwamba matatizo yale ambayo Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na Mhe. Ismail Jussa Ladhu walieleza na mengine waliyoeleza Wajumbe ndio matatizo hasa yaliyosababisha na tukaona kwamba kuna haja ya kuleta sheria hii, ili tuweze kurekebisha baadhi ya mambo.

Lakini Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumza Kitengo cha Usajili na alizungumzia sababu ambazo ya sheria hii hasa katika Kitengo cha Usajili, Mrajis Mkuu. Mhe. Naibu Spika, nafikiri hapa kidogo tatizo ni kwamba hatuzungumzii Mrajis Mkuu, isipokuwa tunachokizungumzia hapa ni mrajis wa shughuli zote hapa, yaani ni tofauti kabisa tunapozungumzia na Mrajis Mkuu ambaye yuko katika maelezo mengine.

Sasa tunapozungumzia ile Sheria ya Mawakala au Uwakala pale ndio tutazungumzia suala la Mrajis Mkuu, ambapo tumemzungumza kwa jina jengine Mkurugenzi Mtendaji na sababu zetu tutatoa kwa nini tukasema Mkurugenzi Mtendaji.

Mhe. Naibu Spika, hii ni kwa sababu tunazo sheria nyingi ambazo zote zina warajis, hivyo tukiwa na sheria nyingi ambazo zote zina warajis, basi lazima kuwe na mtu atakuwa yeye ndiye mwenye kushughulika au mwenye dhamana wa shughuli zote zile za urajis. Lakini hii namuomba Mhe. Hamza Hassan Juma asubiri mpaka pale ambapo tutazungumzia ile Sheria ya Uwakala, ambapo hii tutaelezea kwa uzuri zaidi.

Vile vile Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumzia kuhusu chombo kisichojitegemea, ambapo tayari tumeshazungumzia ile tofauti baina ya *partnership* na kampuni, kwamba *partnership* kile chombo chenyewe kinakuwa hakina dhamana, *liability* zote ziko kwa watu wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, pia alizungumzia kuhusu suala la mashirika ya serikali kuna utaratibu gani. Katika sheria hii tulisema kwamba mashirika ya serikali nayo yatahusika na tulisema hivi makusudi kwa sababu lengo hasa ni kutaka kujua kwa Zanzibar kuna mashirika mangapi au kampuni ngapi.

Sasa zote hizi zikiwa chini ya mwamvuli mmoja basi tunaweza tukajua na hapo tunaweza kupata katika suala zima la kutizama fedha kwa mfano tunazoweza kupata na utaratibu gani wa kufanya, ili mashirika pamoja na kampuni zetu na jumuia hizo ambazo zinahusika katika usajili huu ziweze kwenda sambamba kwa mujibu wa sheria.

Pia tulipata suala kwamba je wizara inajiandaa vipi katika utekelezaji wa masuala haya. Mhe. Naibu Spika, napenda niseme tu kwamba sheria hii kama nilivyosema mwanzo kuwa ina lengo baadaye la kuunganisha huu utaratibu mzima wa mtandao.

Kwa hivyo, tunapofanya hivyo kwa kweli itasaidia sana kuhakikisha kwamba zile kampuni zote ambazo zimekuwa *registered* yanaonekana kwenye mtandao na yanalipa kodi zinazohusika. Kwa mfano, hivi sasa tuna *experience*

kwamba baadhi ya kampuni ambazo zimekuwa *registered* zina matatizo na wala hatujui *details* zake na pengine zinakwepa baadhi ya mambo ya kodi na ushuru.

Sasa tukifanya hivi na huu ndio mwanzo kwa sababu baadaye tunalo lengo la kuunganisha *records* hizi katika mtandao na mtu akiwa na ile *pin* au *tin number* yake, basi unapokwenda popote pale unaweza kuonekana kwenye vitambulisho vile vya *NIDA, ZID* pia ukaonekana kwenye mtandao mwengine wa ulipaji kodi wa *ZRB* na sehemu kama hizo.
Mhe. Naibu Spika, hii kama nilivyosema itasaidia katika utaratibu huo na wala haina maana kwamba zile kampuni ambazo hivi sasa zimeshakuwa *registered* kwamba wao watalipishwa baada ya mwaka mmoja. Kwa hivyo, kama nilivyosema mwanzo kwamba kampuni hizi hazitalipishwa wakati wa ku-*register* baada ya kipindi cha mwaka mmoja.

Lengo ni kuwapa nafasi kwa kipindi kile cha mwaka mmoja, ili waweze kukamilisha mambo yao pamoja na utaratibu ambao utatoka baada ya sheria hii kupita pengine utaratibu mpya na kanuni mpya, ambazo zitawalazimu wao wajaze baadhi ya mambo, kwa ajili ya kukamilisha zile taarifa ambazo zinahitajiwa.

Mhe. Marina Joel Thomas alizungumzia kuhusu kifungu cha 9(2). Lakini hapa napenda nimjibu kwamba madhumuni hasa ya kifungu cha 9(2) ni kurahisisha usajili na kuweka *records* zile ambazo zinatakiwa. Kwa kweli kama nilivyosema mwanzo kwamba hivi sasa baadhi ya kampuni tena ni nyingi hazina *records* zinazotakiwa na hizo zinatupa matatizo katika suala zima la kufuatilia kampuni hizo.

Mhe. Fatma Mbarouk Said, kama nilivyosema kwamba nakubaliana naye kwamba zitumike hizo *tin number*. Lakini katika kutumika hizo *tin number* kama vifungu cha 11 na 18 vinavyosema, kwamba hizi zitatumika kwa utaratibu maalum na mrajis hataruhusu kusajili jina ambalo kwa mfano linalingana na jina linalotumiwa na taasisi nyengine.

Sasa kama hatafanya hivyo kwa kutumia ile *tin number* tu inaweza kuleta matatizo, lakini ni lazima zile *details* zote ziwekwe katika utaratibu ambao kwa mujibu wa kifungu cha 8 kwamba kutakuwa na fomu maalum ambazo fomu hizi kama alivyouliza Mhe. Asaa Othman Hamad hazitakuwepo kwa Sheha.

Kwa hivyo, fomu hizi zitakuwepo ofisi ya usajili na fomu hizi zitakuwa ni kanuni ambazo zitatungwa na Waziri anayehusika kwa wakati huo. Kwa maana hiyo, ni fomu ambazo zitapatikana katika ofisi ya usajili kwa shughuli hizi na wala hazitakuwepo kwa Sheha.

Mhe. Asaa Othman Hamad yeye alizungumzia suala la fomu kama nilivyosema kwamba fomu hizi kwa mujibu wa kifungu cha 23(2) ni fomu ambazo zitaambatana na mambo mengi ambayo yameelezwa kwenye fomu hii.

Kwa mfano, Waziri anatakiwa kutengeneza kanuni kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji mzuri wa sheria hii na kwenye kanuni hizo ni pamoja na fomu zitakazotumika chini ya sheria. Pia kutakuwa na mambo mengine kama vile utaratibu wa kusajili biashara ya mtu mmoja au ubia, utoaji wa taarifa, utaratibu wa ukaguzi pamoja na mambo mengine mbali mbali.

Kwa hivyo, haya yote yatakuja kama ni kanuni za usajili. Kwa maana hiyo, fomu hizi pamoja na fomu nyengine ambazo zitafanywa zote zitatoka katika ofisi ya msajili na wala hazitatoka kwa Sheha au mtu mwengine yeyote.

Mhe. Saleh Nassor Juma na yeye alizungumzia mambo, lakini kama nilivyosema Mhe. Naibu Spika, kwamba mambo haya aliyoyazungumzia Mhe. Mjumbe ni mambo ambayo kidogo yalibadilishika, kwa sababu yeye alizungumzia madhumuni na sababu zilizomo katika sheria hii.

Lakini ukiisoma sheria hii chini ya madhumuni na sababu vile vifungu vyote ambavyo vimewekwa kuanzia kifungu cha 1, 2 na 3 haya yote yanahusiana na wakala, yaani sheria ambayo itakuja baadaye. Kwa mfano, kuanzisha kisheria Wakala wa Usajili wa Biashara au kuimarisha uwajibikaji ndani ya afisi ama kuhakikisha kuwa kazi za wakala zinafanywa na wafanyakazi wenyewe.

Sasa hii hatujazungumzia katika sheria hii, kwa bahati mbaya kama nilivyosema mwanzo, kwamba hii ilikuwa iwekwe katika sheria ile ambayo itazungumzwa baadaye na yale maelezo ya madhumuni na sababu yalioko katika

sheria ile sehemu yake ilikuwa yaje kwenye sheria hii. Kwa hivyo, kuna *confusion* hiyo kidogo, hivyo kwa hili kama nilivyosema mwanzo wakati nilipokuwa niki-*introduce* sheria niliomba radhi Wajumbe kwa usumbufu huo.

Lakini lengo hasa la sheria hii tunayozungumza ni suala zima la usajili wa hizi kampuni ambazo hivi sasa zimesajiliwa, lakini zimesajiliwa katika sheria mbali mbali. Kwa mfano, kama nilivyosema kuna sheria ambazo zimesajiliwa chini ya sheria za kampuni, kuna mambo mengine yamesajiliwa chini ya jumuia, pia kuna mambo mengine yamesajiliwa chini ya vyama vya ushirika.

Kwa hivyo, zote hizi unapotaka taarifa na kwa sababu usajili unafanywa na watu tofauti, hivyo zile taarifa hasa huwezi kuzipata zote za uhakika. Kwa mfano, unapochukua kampuni ambayo imesajiliwa chini ya sheria za kampuni, halafu ukachukua kampuni iliyosajiliwa chini ya jumuia pengine taarifa utazipata tofauti wengine watajaza hivi na vile na tutakuwa na matatizo kidogo. Lengo ni kufanya zile kampuni zote ziwe chini ya mwamvuli mmoja na ziwe zinaweza kutizamwa, kama kuna mambo ya kukosolewa zinaweza kukosolewa kwa umoja na zaidi ni kurahisisha usajili wa biashara.

Kwa kweli siku hizi Mhe. Naibu Spika biashara imekua sasa mtu mwenye kampuni hatapenda kusumbuliwa sana kwenda huku na kule. Hivyo, tukizifanya kwa pamoja hapa chini ya mwamvuli mmoja inaweza kusaidia na hili jambo kubwa ni kwamba itasaidia serikali pia kupata *fee* hii, kwa sababu hivi sasa watu wengi kutokana na usumbufu ambao tunao wanasajili kampuni zao mahala mwengine kama vile Bara na hata nchi nyengine.

Lakini kwa mujibu wa sheria zetu hivi sasa unaruhusiwa kuja kufungua *subsidiary company* na ufunguaji wa *subsidiary company* fedha ambazo zinapatikana ni kidogo. Mhe. Naibu Spika, tukiyafanya haya yote kwa pamoja na yakawa ni rahisi kuyafanya kwa wakati mmoja na muda mfupi, basi naamini watu wengi watasajili kampuni zao kwa utaratibu mpya ambao tutauweka na fedha nyingi tunaweza kuzipata ukilinganisha na nyuma.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo niwaombe tena Wajumbe, kwamba suala hili ni muhimu katika misingi hiyo ambayo nimeeleza na ninaomba mukubali kwamba mswada huu upitishwe, ili uwe sheria. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria, ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara Zanzibar ya 2012

Sehemu ya Kwanza
Masharti ya Awali

Kifungu 1

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimshukuru Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake mzuri aliotutolea. Kwa kweli kama tulivyosema tokea jana kwamba mswada huu ni wa kitaalamu sana na uko *very complicated* maana yake kwa sababu umegusa mambo mengi. Sasa tulikuwa tunataka ufafanuzi zaidi, ili tunapopitisha hii sheria wananchi wetu wakituuliza jambo lolote kuhusu sheria hii tuwe na uelewa mzuri, kwa hivyo naamini Mhe. Waziri ataweza kunijibu ili niridhike.

Swali langu linakuja kwamba sheria hii ni sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara Zanzibar na itaanza kutumika, yaani nakusudia ile tafsiri ya usajili na kama tunavyofahamu kwamba kuna taasisi nyingi ambazo tumezitungia sheria kwa ajili ya kusajili.

(a) Je, zile taasisi nyengine ile kazi ya usajili tukishapitisha sheria hii, kwa hiyo ina maana kule ule usajili unafutika moja kwa moja.

(b) Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la usajili kila taasisi au kampuni au kila ushirika inataka iwe na wataalamu wanaojua.

Mfano tuchukulie kama ile Bodi ya Wakandarasi, pale Bodi ya Wakandarasi inasajiliwa na wale wenye ile bodi inayoshughulikia wakandarasi. Ina maana pale kuna vigezo vya mpaka kuridhika na kukubali kwamba hii sasa hivi tunaweza tukaipa usajili kama ni kampuni. Maana unaweza ukaambiwa iwe na wataalamu wa aina fulani na aina fulani. Mfano kama kwenye wawekezaji, kwenye mahoteli kunatakiwa hivi na hivi. Sasa wizara itakuwa tayari imeshajiandaa na kuwa na wataalamu wote hao kwa kuwa *central* katika hilo eneo ili taasisi yoyote inayotaka kuja kusajiliwa pale iwe ule uwelewa wa usajili wanao hao wataalamu au hii taasisi ambayo itakayopewa hayo mamlaka.

Jengine Mwenyekiti katika suala zima la usajili, inawezekana kwamba kuna kampuni ya ujenzi inataka kusajiliwa. Lakini vile vigezo vinavyotakiwa vya wataalamu ili ile kampuni iweze kusajiliwa havikutimia. Je, hii Mamlaka yetu ya Usajili itakuwa na uwezo wa kuikatalia usajili. Mfano pengine kuna kampuni au taasisi ambazo tayari zimeshasajiliwa lakini kumbe hazikutimiza vile vigezo ili ile kampuni isajiliwe. Je, Mamlaka hii itakuwa na uwezo wa kuweza kuzifuta zile. Kidogo nilikuwa nataka nipate maelezo ili tupate hii tafsiri halisi ya hichi ambacho tunachokipitisha. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli maswali ya Mhe. Hamza Hassan Juma ni mazuri na yatasaidia sana katika kuelimisha zaidi. Kwanza ukisoma kifungu cha pili cha huu Mswada inasema wazi kwamba sheria hii itatumika sambamba na sheria zinazosimamia usajili na uendeshaji wa taasisi zifuatazo. Kwa hivyo sheria hii itakwenda pamoja na sheria zinazotawala masuala haya tuliyoyataja, makampuni, jumuia, vyama vya ushirika na kadhalika, kwa hivyo sheria hizi zitakwenda pamoja. Kule kutakuwa na usajili, lakini lengo hapa kama nilivyosema mwanzo ni kudhibiti. Kwa maana hiyo ukisoma kifungu cha 23 kinasema kwamba "waziri anayehusika atafanya kanuni" ili zile kanuni ndio zitakazoongoza ule mwenendo mzima wa usajili. Wakati huo huo usajili na sheria nyengine zinahusika.

Kwa hivyo utaratibu sasa utawekwa mtu akitaka kusajili kwa mfano chini ya sheria ya kampuni kutakuwa na utaratibu gani na utaratibu gani. Kwa maana hiyo huu usajili huu utatizama zile sheria ambazo zipo hivi sasa katika kusajili hizo kampuni. Hizo zitakwenda sambamba na zile kanuni ambazo zitakuwa zimeshawekwa. Mhe. Mwenyekiti, cha muhimu hapa kwamba sheria hii ikipita kuna umuhimu wa haraka wa kufanya hizo kanuni ambazo zitatawala usajili wa shughuli hizi.

La pili Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria hii msajili anaweza akakataa ikiwa zile kanuni au ule utaratibu uliyokuwepo kwenye kanuni hazikukamilishwa anaweza akakataa. Akikataa sheria hii inasema kwamba ni lazima atoe sababu kakataa kwa sababu gani ili yule aliyokuwa anasajili aweze kujua kakataliwa kwa sababu hii na hii.

Swali lake la tatu ni kweli kwamba kama kuna kitu ambacho kinakwenda kinyume na ule utaratibu basi pia kuna uwezo wa kufuta ili isiweze ikaleta matatizo. Nakushukuru Mheshimiwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake nilikuwa nahitaji maelezo ya ziada kidogo mfano. Pengine kuna kampuni ambayo imesajiliwa katika taasisi ambayo ipo kisheria lakini baada ya sheria hii kufanya kazi kama ilivyoelezwa kwamba baada ya kutiwa saini, pengine ikaonekana kwamba kampuni tayari inafanya kazi lakini kumbe yale masharti yanayotakiwa kuisajili ile kampuni hayakutimizwa. Je, hapa kuna hatua gani, kwa sababu hapa tayari kama alivyojibu Mhe. Waziri kama hawakutimiza masharti wanaweza wakaikataa na huku pengine kampuni imeshasajiliwa, ila tu ni kutokana na sababu za hapa na pale hawakutimiza yale masharti, lakini wao baada ya kuja kutathmini wakagundua yale masharti hayakutimia.

Mfano kama nilivyozungumzia ma-*contractor* hawa vile vigezo vya wataalamu na mambo mengine. Je, kama kampuni tayari imepewa kazi inafanya hawa wakija wakitaka kuusisha ule usajili wake hali itakuja kuwaje.

Jengine sheria hii inasema kwamba itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri ataitangaza katika gazeti rasmi. Huku katika kifungu cha 23 kama alivyosema kwamba Mhe. Waziri ataandaa kanuni za kuandaa muongozo au mambo madogo madogo ya kuweza kuhakikisha kwamba kazi zao wanazitekeleza vizuri. Mimi hofu yangu hapa hii sheria inaweza ikachelewa sana kutangazwa katika gazeti rasmi kwa sababu kuna kanuni ambazo Waziri atakuwa bado hajazitunga ambazo zitakazokuwa kama ni muongozo wa utekelezaji wa sheria hii.

Sasa je, hapa Mhe. Waziri atatuthibitishia vipi kwamba hii sheria hasa kwa kuwa inakwenda sambamba na hizi sheria nyengine lazima itabidi utoke muongozo wa kimaandishi unatoka kwa Mhe. Waziri. Je, atatuhakikishia vipi kwamba hizi kanuni wamejiandaa kwa muda gani zitaweza kutungwa ili hii sheria ije itekelezeke vizuri. Kwa sababu sheria tunajua tukishakuipitisha hapa Rais ataitia saini ina maana itakuwa sheria kamili. Lakini huku kanuni hasa kwa sheria hii lazima kanuni itakuwa ndio kitu muhimu ambacho kitakachokuwa kinaongoza sheria hii. Sasa labda Mhe. Waziri anisaidie tena hapo kidogo. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza swali lake la mwanzo kwamba madhumuni ya kusema zile Kampuni ambazo zimeshasajiliwa zipewe mwaka mmoja na pamoja na kukamilisha hayo maelekezo yatakayokuwepo katika kanuni zitakazofanywa hiyo ndio moja.

Sasa ikiwa kampuni imeshapewa mwaka mmoja na haikutekeleza kifungu cha 24(3) kinatoa adhabu na kwamba inaweza hata kampuni yake ikafutwa.
La tatu ni kwamba je, hii sheria inasema itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri ataitangaza katika gazeti rasmi. Utaratibu wa sheria tunajua kama itapita hapa halafu inakwenda kwa Mhe. Rais kwa kupata kibali chake. Ikishakupata kibali chake kwa mujibu wa sheria hii ndiyo waziri sasa anatakiwa aitangaze tarehe ya kutumika.

Napenda nimuhakikishie Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba hivi sasa sisi Idara inayohusika na Wizara tumeshaanza kuzikalia hizi kanuni na ya kuzifanya. Namuhakikishia kwamba inapotiwa sahihi tu hii na tukaitangaza tarehe ya kutumika naamini baadhi ya kanuni ambazo ni muhimu zitakuwa tayari. Nakushukuru.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nilisema nifafanue jambo moja dogo tu kwa vile Mhe. Hamza Hassan Juma alichotaka ni ufafanuzi ambao utawasaidia wananchi pamoja na Waheshimiwa humu ndani ili kuweza kufahamu kuhusiana na sheria hii, sasa ana wasi wasi na kwa sababu aliuliza kitu na sijui kama na yeye mwenyewe amekifahamu vizuri.

Maana aliuliza kwamba kuna kampuni kwa mfano *contractors* wamesajiliwa na Bodi ya Mkandarasi, sasa kule kuna masharti yake, huku kwa Mrajis huyu yatazingatiwa vipi yale masharti ya kule kwa bodi ya wakandarasi na inawezekana pengine mtu katimiza masharti huku kusajiliwa kama kampuni lakini kule inawezekana vile vigezo havijatimizwa. Je, hapa kutakuwa na uhusiano gani baina ya hizi taasisi mbili.

Mhe. Mwenyeki, suala la msingi ni kwamba katika usajili wa taasisi ya biashara kuna hatua mbili na hili ni vizuri tulifahamu vizuri sana. Kuna hatua ya kwanza ndiyo tunaiita ya kuzaliwa. Yaani usajili kwa sababu kwa mfano kama Kampuni, kampuni ni kama binaadamu ndio maana tumemuita kwenye sheria ni mtu wa kutengeneza. Sasa kama ni mtu wa kutengeneza ina maana lazima atengenezwe, yaani azaliwe kama binaadamu wa kimaumbile anavyozaliwa na hii taasisi ya biashara lazima ifike kwanza pahala izaliwe.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kampuni imeshazaliwa, ikishakuzaliwa hii bahati nzuri hii kamapuni inakuwa kama vile wanyama wengine wakishazaliwa wanaanza kukimbia. Kampuni nayo baada ya kuzaliwa suala linalofuata inataka kufanya biashara gani. Kwa mfano kama anataka kufanya biashara ya *contractor* sasa inabidi aende kwa yule anayadhibiti usajili wa wakandarasi, kule sasa akapewe masharti ya kule ili aweze sasa kufanya hiyo biashara ya ukandarasi. Au anataka biashara ya kutoa mizigo bandarini kwa hivyo inabidi aende kwa ile mamlaka inayodhibiti utoaji wa mizigo bandarini atimize masharti ya utoaji mizigo bandarini.

Hapa katika sheria hii kinachofanywa ni udhibiti wa kuzaliwa hizi taasisi zenyewe, kamka watu mwengine anazaliwa Mnazimmoja, mwengine anazaliwa Mwembeladu na pengine kwa watu ni rahisi lakini kwa hizi sheria kwa kampuni au taasisi za biashara imekuwa ni tatizo, majina yanaleta *confusion*, kazi zao zinaleta *confusion*, mfumo wao wa kodi unaleta *confusion* ndio maana kama vile serikali ingeweza kutangaza kwamba watu wote wakazaliwe Mwembeladu, sasa na hii ndio tunasema badala ya kila mtu kwenda wizara au shirika au kwengineko basi sasa wote wanatakiwa waende pahala pa kuzaliwa ni pahala pamoja.

Lakini wanataka kufanya nini baada ya pale inategemea hizi mamlaka. Kwa hivyo hizi mamlaka za udhibiti wa zile biashara bado zitaendelea kuwepo. Lakini atakuwa anajulikana hizi katika uzazi wao katika masharti yao ya kuzaliwa basi yatakuwa ni pahala pamoja na kumbukumbu zao zitaweza kupatikana pahala pamoja na udhibiti wao utakuwa pahala pamoja kwa suala hili la kuwepo kwao katika mfumo wa utendaji. Ahsante.

Kifungu 2 Matumizi ya sheria.
Kifungu 3 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Pili
Uanzishwaji wa Masjala Taasisi za Biashara

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, jana nilipokuwa nikichangia nilisoma madhumuni na sababu ya Mswada huu ni kutunga sheria itakayoanzisha wakala wa usajili wa biashara na mali.

Tatizo langu nilisema kwamba hizi mali mali kwa sababu mali zipo za mpito, mali za kudumu. Nilitaka Mhe. Waziri anisaidie kidogo kuhusu hizi mali ni mali gani. Kwa sababu kuna mali nyingi kwa mfano hata mimi na wewe tutakuwa ni mali kwa wanaotumiliki pengine kwa hivyo isije ikawa ni tatizo hapa. Kwa hivyo nilikuwa namuomba Mhe. Waziri anifafanulie ni mali za aina gani.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nilisema hapa kwamba haya madhumuni na sababu tusiyatizame sana kwa sababu yalibadilika. Hili suala la wakala lipo katika sheria ambayo tutaizungumza baadaye. Kwa hivyo hapa halihusiani na suala la wakala hapa ilikosewa tu katika uandikaji.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 4 Uanzishwaji wa masjala, taasisi za biashara pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 5 Kazi za masjala pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Tatu
Utaratibu wa Kusajili

Kifungu 6 Maombi ya usajili pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 7 Wajibu wa taasisi ya biashara pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 8 Wajibu wa kutoa vielelezo.
Kifungu 9 Wajibu wa taasisi ya biashara pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 10 Usajili wa taasisi ya biashara na jina la biashara pamoja na marekebisho yake
Kifungu 11 Kuzuia jina na marufuku katika baadhi ya majina pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 12 Kipaumbele katika kutumia jina pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 13 Mapokezi ya maombi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 14 Taratibu za usajili pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 15 Hati ya usajili pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 16 Usajili wa marekebisho pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 17 Uondoshaji wa jina kwenye daftari la usajili.

Sehemu ya Nne
Masharti Mengineyo

Kifungu 18 Taarifa kwa umma
Kifungu 19 Utoaji wa taarifa
Kifungu 20 Mjumuiko wa makosa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 21 Adhabu ya jumla pamoja na marekebisho yake
Kifungu 22 Makosa yanayowahusu Maofisa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 23 Kanuni pamoja na marekebisho yake
Kifungu 24 Uwekaji sawa taarifa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 25 Marekebisho yatokanayo pamoja na marekebisho yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali Mswada huo. Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria wa Usajili wa Taasisi za Biashara
Zanzibar ya Mwaka 2012

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria wa Usajili wa Taasisi za Biashara Zanzibar ya Mwaka 2012 usomwe mara ya tatu.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Katibu: Mswada wa Sheria wa Usajili wa Taasisi za Biashara na mambo mengine yanayohusiana na hayo pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Mswada wa Sheria wa Usajili wa Taasisi za Biashara na mambo mengine yanayohusiana na hayo sasa umepitishwa rasmi na Baraza lako tukufu la Wawakilishi Zanzibar kuwa ni sheria. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mswada umepitishwa.

Waheshimiwa Wajumbe kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa ushirikiano mlionipa mimi pamoja na Waziri na hatimaye tumeupitisha Mswada huu muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Kabla sijaakhirisha kikao naomba nitoe matangazo mawili.

1) Tulipata taarifa ya kuwa na semina katika Baraza letu hapa kesho, lakini kwa bahati mbaya tunaomba tutangaze kwamba semina hiyo imeakhirishwa kwa mambo ya msingi sana. Kwa hivyo Jumatatu mtapewa taarifa kwamba tutafanya lini semina hiyo.

2) Pili nisisitize kwamba Jumapili wanakuja wenzetu wa Tume ya Kurekebisha Katiba. Sasa naomba Tume watukute sisi saa 3:00 sio Tume watungoje wao. Tujitahidi kuja mapema ili wakija wao watukute, itakuwa si jambo zuri kwamba sisi tuwakute wao. Kwa sababu ukimualika mgeni nyumbani wewe ukenda kondeni mgeni ukimkuta anakusubiri inakua kidogo haina nidhamu. Kwa hivyo nasisitiza tujitahidi tufike mapema ili wakija wao tuwapokee. Nadhani hapo tumefahamiana.

Baada ya matangazo hayo sasa naomba kuakhirisha kikao chetu hichi hadi siku ya Jumatatu tarehe 15/10/2012 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 5:45 asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 15/10/2012 saa 3:00 za asubuhi)